# *Njia Panda Ya Wakati*

Ninataka wanaorekodi waushikilie huu kwa muda mfupi kabla hamjarekodi, tafadhali. Na habari za asubuhi, marafiki. Natumaini kuwa kila mtu anajisikia ninii sana. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

2 Tuimbe wimbo wetu rasmi wa kuweka wakfu, *Waleteni*, kila mtu pamoja sasa, "Waleteni watoto wadogo."

> Waleteni, waleteni,
> Waleteni kutoka maeneo ya dhambi;
> Waleteni, waleteni,
> Waleteni watoto wadogo kwa Yesu.

3 Amina. Hivi hamwazii kuna kitu cha kupendeza sana kuhusu mtoto mchanga? Jamaa mdogo, hayo macho madogo, maangavu yanayonitazama. Na kuna kitu fulani juu yao ambacho ni cha kupendeza sana, sana. Nao ni watoto wadogo tu wasio na hatia, hawajui lolote kuhusu mambo ya ulimwengu. Mungu ametoa.

4 Na, mnajua, kuna kitu fulani kuhusu mtoto, nyumbani, ambacho hufunganisha hiyo nyumba pamoja. Kuna kufungamana, kuhusu mtoto. Sasa, laiti tungalikuwa na wakati zaidi wa kuongea juu ya—juu ya mambo hayo, kuhusu watoto wadogo, na kuhusu mambo mbalimbali. Lakini sisi, wakati wetu, tunaushidania sana wakati.

5 Nasi hatuna budi kuliendea Neno moja kwa moja sasa. Sawa, kwa wanaorekodi, kama wakitaka kurekodi ujumbe asubuhi ya leo. Na Mungu ambariki sana kila mmoja.

6 Sasa, leo, nafikiri hakuna kitu kama Neno, kusomwa kwa Neno la Mungu. Laiti ingekuwa katika kila nyumba, ambako Neno la Mungu lingesomwa. Nami nataka kila mmoja wenu, asubuhi ya leo, kama mkiweza, hata watoto watakapotoka katika vyumba vyao vya shule ya Jumapili, wawe na uchaji tu iwezekanavyo. Waketi kimya, na wasikilize ninapojaribu, kwa msaada wa Mungu, kuleta Ujumbe niliopewa usiku sana jana usiku, kwa ajili ya kanisa leo hii.

7 Sasa, somo letu la Maandiko linapatikana katika Yoeli 2, na Matendo 2, Yoeli 2:28. Katika Matendo, tunaanzia kwenye 2:15. Si ni ajabu, ambavyo nabii huyu, akizungumza, mlango wa pili wa Yoeli, na mlango wa pili wa Matendo, "mvua ya masika na ya vuli," Yoeli alizungumza juu yake katika mlango uu huu! Kwa kunena kutoka katika Matendo, mlango wa pili, kifungu cha 15, na sehemu ndogo ya Maandiko, tunasoma hivi.

> *Sivyo mnavyodhania, watu hawa hawakulewa, kwa maana* ni *saa tatu ya mchana.*

*Lakini jambo hili ni lile lililonenwa na nabii Yoeli;*

*Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho yangu:. . .wana wenu na binti zenu watatabiri, . . .vijana wenu wataona maono, na* juu. . .nao *wazee wenu wataota ndoto:*

*Naam, na siku zile nitawamwagia watumishi wangu, wanaume na* wanawake, *Roho yangu; nao watatabiri:*

*Nami* nitaonyesha *maajabu katika* mbingu *juu, na ishara katika nchi chini; damu na moto, na mvuke wa moshi;*

*Jua litageuka kuwa giza, na mwezi kuwa damu, kabla ya kuja ile siku ya Bwana, iliyo kuu na iliyo dhahiri:*

*Na itakuwa kila atakayeliitia jina la Bwana ataokolewa.*

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi.

8 Baba yetu wa Mbinguni mwenye fadhili, kama shuka kubwa kwenye jengo hili asubuhi ya leo, kila kichwa kikishuka kwenye mavumbi ya nchi. Kwa unyenyekevu tunainamisha vichwa vyetu na mioyo yetu, katika Uwepo Wako. Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, kwamba Roho Mtakatifu atakuja sasa, aingie katika Neno, na kuliwasilisha kwa kila moyo ulio na nafasi, na mahali pa kukaa. Jalia lizae mara mia. Mungu, tunaomba kwamba wasioamini, leo hii, waweze kuwa waaminio. Na kwamba Wakristo watapata mshiko mpya, wale walio wachovu safarini. Watakatifu na watiwe moyo, na wagonjwa wapone. Nena, Baba. Na jalia tushiriki kwenye Neno Lako sasa hivi, kwa maana tunaomba hayo katika Jina la Mwana mpendwa wa Mungu, Yesu Kristo. Amina.

9 Somo langu, asubuhi ya leo, kama tungeliita hivyo, litakuwa ni ujumbe kwa kanisa, ni: *Njia Panda Ya Wakati.*

10 Na sikuzote, katika siku zilizopita, vipindi vya nyakati siku zote vimefikia mwisho wake, nasi tunafikia njia—njia panda. Kuna njia panda kwenye barabara kuu. Kuna njia panda kwenye barabara ambazo tunasafiria katika ulimwengu huu. Kuna njia panda kwenye barabara hii kuu ya kale tunayosafiria kwenda Utukufuni.

11 Na, daima, inahitaji mambo ya kimiujiza kunena juu ya uweza yote. Mwenyezi ndiye mwenye nguvu zote, na inahitaji mambo ya kimiujiza kuthibitisha uweza yote. Na ni ya kimiujiza tu yanayoweza kufanya hivyo. Kufundisha Neno ni jambo zuri sana, na sisi. . .linakuja, "Imani chanzo chake ni kusikia, na kulisikia Neno," lakini sikuzote inahitaji mambo ya kimiujiza kuthibitisha kwamba mweza yote angali anamiliki. Hatuna budi kuwa na mambo ya kimiujiza. Nami ninaamini kwamba Kanisa sasa limesimama langoni mwa uthibitisho mkubwa zaidi

wa uweza yote ambao ulimwengu ulipata kujua. Kumekuwako na. . .

12 Katika uchunguzi wangu wa Maandiko, kwa muda mrefu sana, nimepata njia panda saba kubwa katika Neno la Mungu. Na saba ni namba kamili ya Mungu. Sisi . . . Yeye—Yeye hukamilika katika saba. Alifanya kazi siku sita, na, ya saba, akapumzika. Ulimwengu huishi katika utawala wake juu ya nchi hapa, Kanisa linafanya kazi kwa miaka elfu sita, ya saba ni ule Utawala wa Miaka Elfu. Na hisabati hizi zote (na) za Biblia ni kamilifu.

13 Naye Mungu sikuzote huwa kwenye wakati unaofaa. Wakati mwingine sisi huchelewa kidogo, au (kidogo) tukifikiri tofauti kidogo, lakini hilo hufanywa kila mara kwa kusudi fulani. Lakini Mungu daima huwa kwenye wakati unaofaa na Ujumbe Wake.

14 Na kwa hiyo, leo hii, ninaamini ya kwamba tunakabiliwa na jambo fulani kuu ambalo Kanisa linapaswa kujua na kulifahamu, kwamba tunapaswa kujua haya yote yanahusu nini, na kuyatafuta katika Neno la Mungu. Kwa maana ninaamini, kwamba, kama—kama haliko katika Neno, kidogo nina shaka nalo. Lakini ikiwa Neno la Mungu linalizungumzia, basi Mungu, haidhuru jinsi gani linaweza kuonekana la kutojali kwa desturi yetu ya kufundisha, ni Mungu akilitekeleza Neno Lake. Mara nyingi, ni kinyume na njia yetu ya kuwazia, au labda njia ambayo tumefundishwa kuwazia, lakini inatupasa kutambua ukuu wa Mungu wakati unapoonyeshwa mbele zetu.

15 Sasa hebu turudi nyuma kwa muda kidogo, niani mwetu, na tuchunguze, kwa dakika chache tu, kwa miaka michache iliyopita kile kimekuwa kikitendeka. Ninaamini, kama mhudumu wa Injili, kwamba tunaishi tu kwenye kule kuonekana kunakokaribia, kwa mara ya pili, kwa Kuja kwa Bwana Yesu; kurudi mara ya pili . . . au Kuja Mara ya Pili. Mara ya kwanza, alikuja kama mtoto mchanga. Wakati huu, anakuja kama Mfalme wa Utukufu, kulipiza kisasi juu ya wote wasiolitii Neno la Mungu.

16 Nasi tunaamini, pamoja na misukosuko hii yote mikuu tunayoishi ndani yake, leo hii, tunapotazama kila upande, na kuchukua magazeti, na kusimama tu kimya, na kuachana na pilka-pilka zetu za kila siku za wakati huu wa kiwazimu, na kuangalia na kukabiliana na ukweli wa mambo, tunaona, bila shaka lolote, ya kwamba jambo fulani liko karibu kutukia.

17 Nami naamini ya kwamba Mungu, kamwe, wakati wowote, hakuna cha kimiujiza, ama hakuna kilichowahi kutukia, isipokuwa Mungu alitangulia kukionyesha kwa Neno Lake. Akakifunua, akakiweka mahali pake, ili kwamba watu wanaoshindwa kutembea ndani yake, waweze . . . itawabidi kusimama mbele Zake, na ingebidi awe . . . asimame bila

udhuru, kwa maana Mungu hukiweka wazi kabisa. Kwamba, kama mtu anajali vya kutosha kukihusu, atakipata, kama unajali.

18 Usingekunywa supu iliyo na nzi ndani yake. La, bwana. U—usingeinywa. Usingekuwa . . . Ungeogopa kula chakula ambacho hakikuonekana sawa kabisa, na kilikuwa kimechafuliwa. Kwa sababu, unajua, kinaweza kukupa sumu ya chakula ama chochote kile, na kingekuua baada ya muda mfupi. Na wewe unautunza mwili huu. Lakini, hiyo nafsi, unaiacha ijifurahishe na mambo ya ulimwengu, ambayo unajua yamechafuka na yanaweza tu kufanya jambo moja, kukupeleka kwenye maangamizi. Haijalishi jinsi unavyoutendea vizuri mwili huu, na jinsi chakula kilivyo kizuri, ama jinsi unavyoishi, hauna budi kuingia katika mavumbi ya nchi. Lakini nafsi hiyo itaishi milele, mahali fulani. Afadhali ninywe supu iliyochafuliwa kuliko kuichafua nafsi yangu na mambo ya ulimwengu, wakati wowote.

19 Njia panda! Mungu, daima, kabla ya kuja kwa njia panda hizi kuu, ama kumalizika kwa wakati, ambapo Yeye huanzisha jambo jipya, njia panda za kale, hadi zile mpya, pamoja na kipindi kimoja cha wakati hadi kingine, Yeye daima huonyesha Nguvu Zake. Mwanadamu, kote katika nyakati, daima huvunjilia mbali, na kufundisha vibaya, na kuelezea vibaya, na kumwacha Mungu halisi aliye hai. Lakini, kabla tu Yeye hajaingia kwenye njia panda na kuingia kwenye kipindi kipya cha wakati, Yeye hujitokeza jukwaani, pamoja na ishara kuu za kimiujiza na maajabu. Sikuzote amefanya hivyo.

20 Angalieni maangamizi ya kwanza ya ulimwengu, ile njia panda ya kwanza. Baada ya ulimwengu kuumbwa, na Mungu kumweka binadamu duniani, Biblia ilisema ya kwamba walianza kujenga miji, miradi mikubwa ya ujenzi iliendelea ulimwenguni.

21 Iangalieni siku hizi. Yesu alisema dhahiri, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwake Mwana wa Adamu." Jambo lile lile.

22 Mnaona, walikuwa wamegundua njia ya kufanya kazi na shaba nyekundu. Walikuwa wamegundua njia ya kufanya kazi na shaba nyeupe, na pamoja na chuma, kabla tu ya yale maangamizi yaliyotangulia ile gharika.

23 Angalieni siku tunayoishi sasa, jinsi ambavyo mijengo! Walisema, "Watu wakaongezeka juu ya uso wa dunia." Angalieni kote ninii yetu . . . hata mji wetu mdogo, na kulinganisha mji huu mdogo, miaka michache iliyopita, wa watu elfu kumi na nne, sasa karibu elfu ishirini na saba au zaidi. Hata huwezi kupata angalau mahali pakubwa vya kutosha kuwindia sungura, tena. Pote ni mradi wa ujenzi wa nyumba. Hiyo ni kweli. Mijengo! Kuongezeka! Kuzaana!

24 Naye akasema, "Walipoanza kuongezeka, ndipo dhambi na uovu ukaingia." Hiyo ni mojawapo ya vibao vikuu vya kuelekeza, kwamba tumefika mwisho wa safari; moja ya ishara kuu.

25 Angalieni, mnamo wakati huo, palikuwa na mtu mmoja jina lake Nimrodi, aliyetoka akaenda kuujenga ule mji mkubwa wa Babeli, na kuiunganisha miji yote jirani, kwamba wote waungane pamoja. Ndipo kungekuwako na jiji moja kubwa, nalo lingekuwa ni Babeli. Na jinsi ambavyo Mungu alilidharau shirikisho hilo la utaratibu wa ulimwengu!

26 Liangalieni siku hizi, jambo lile lile. Mashirika ya wafanyakazi, watu wakijifungamanisha pamoja kwa vyama vya wafanyikazi na kwa—kwa pingu mbalimbali, na kwa madhehebu ya kanisa. Linawafungamanisha wote pamoja, linavunja kizuizi, linavunja u—ushirika kati ya ndugu mbalimbali. Shirikisho, moja ya ishara kuu ambazo Mungu alitoa katika ule uharibifu wa kwanza, tunaiona ikitokea hapa katika uharibifu wa mwisho. Mnaiona?

27 Angalieni, na jambo lingine alilofanya huko nyuma, tunaliona wakati wa machafuko haya makubwa, wakati mioyo ya watu inapoanza kupoa na kumwacha Mungu, wanawake wakawa kijimungu kikubwa. "Wana wa Mungu walipowaona hao mabinti za wanadamu, ya kuwa ni wazuri—wazuri," ikawa ni mambo ya kujuana kimwili.

28 Yaangalieni siku hizi, yale tunayoishia. (Sio kuwakashifu wanawake wa heshima. La, bwana. Hao ni vyombo vya Mungu.) Lakini wale wasiojijali; jinsi kulivyo na wengi upande huo mwingine, wakiendelea, "wakioa, kuolewa." Mungu alisema hivyo, katika Biblia. Yesu alisema, "Kabla ya wakati wa Nuhu," mwishoni, "walikuwa wakioa na kuolewa." Jinsi ambavyo hayo machafuko makubwa yalivyo duniani siku hizi! Nasi tunatambua hilo. Na jambo moja lililosababisha hilo, Biblia ilisema ya kwamba pepo (roho wakuu) walishuka, pepo wachafu, na kuwaingia watu hawa na kufanya mambo haya. Nasi tunaona pepo hao hao wachafu wakifanya kazi katika siku zetu.

29 Na sasa angalieni tena, hilo, si hilo tu. Wakati kuzimu yote inapofunguka, Mbingu yote inafunguka, pia. Adui anapoingia kama mafuriko, Roho wa Mungu huinua kiwango dhidi yake. Na nguvu hizi mbili sikuzote zilijitokeza kwenye njia panda.

30 Sasa, tunapoona ya kwamba wakati ambao Nimrodi alikuwa ameleta shirikisho lote pamoja, na kuwafanya watu wote waje Babeli na kuingia katika shirikisho hili kuu, na wakati wa huo uovu wote kuendelea kati ya wanawake, kujuana kimwili, na kadhalika; wakati uo huo, Mungu alikuwa na shahidi duniani: Henoko, ambaye alitembea pamoja na Mungu, bila lawama. Na wakati uo huo uovu ulipokuwa ukitokea, malaika walitokea duniani. Viumbe wa kimalaika walihamia kwa mwanadamu.

31 Mfano mzuri sana wa siku hizi, pia. Wakati uovu unapotokea, vivyo hivyo mema yanatokea.

32 Basi angalieni huko nyuma katika siku hizo ovu, kabla tu ya yale maangamizi, wakati Mungu alipokuwa na mtu huko nje akiihubiri Injili, mtu maskini, mtu mnyenyekevu, si wa kilimwengu sana, bali mtu aliyekuwa na moyo wa kumsikiliza Mungu; Nuhu. Kulikuwako na Nuhu na Henoko, wakihubiri, wakati ule ule.

33 Na kama ukiangalia, huko katika Ufunuo 11, ilisema, "Nitawaruhusu mashahidi Wangu wawili katika siku za mwisho," mashahidi wawili tena katika siku za mwisho, Ufunuo 11, "nao watafanya ishara na maajabu miongoni mwa watu."

34 Angalia huko nyuma basi, wakati Nuhu na Henoko walipokuwa wakihubiri. Naye Nuhu alikuwa akihubiri ujumbe ambao ulionekana wa kiwazimu sana kwa ulimwengu. Naye Nuhu. . .Hili hapa sasa. Nuhu alikuwa akiandaa safina, akitengeneza mahali pa usalama. Nao huo wenyewe ulikuwa ni muujiza. Jinsi ambavyo mtu, juu ya nchi kavu, ambapo maji hayakuwa yamewahi kuja kamwe, alikuwa akiandaa safina ya kuelea juu ya bahari kuu ambayo ingetokea huko. Na kusema, "Yatashuka kutoka angani," nayo yalikuwa wapi? "Lakini kwa imani," ambayo yenyewe ni mwujiza, "Nuhu, akiisha kuonywa na Mungu, aliandaa safina." Mnaliona? Haidhuru ilionekana ya kijinga jinsi gani, jinsi ilivyoonekana ya kilokole, kwa watu; ilikuwa ni mwujiza, yenyewe, kumwona mtu akiendelea kupiga nyundo. Kwamba kitu fulani kilionekana cha kilokole.

35 Imejirudia tena leo. Huku watu wakiieneza Injili ya Bwana Yesu Kristo kwa dhati, wakihubiri ubatizo wa Roho Mtakatifu, wakiwatayarisha watu kwa ajili ya hukumu zijazo, au kinga dhidi yake. Nao watu wa kanisa la kisasa wakicheka na kufanya mzaha, na kusema, "Hakuna kitu Kwake. Na siku za miujiza zimepita." Ni mwujiza, ubao wa kuelekeza kwenye njia panda.

36 Nuhu, akifanya kazi kwa nguvu, si kwamba tu alikuwa. . . kufanya mwujiza, au kuangalia. . .Alikuwa akiutarajia, pia, mwujiza.

37 Nalo kanisa siku hizi, linapojishughulisha sana na kazi ya kuihubiri Injili, huku ishara na maajabu yakifuata, wanajiandaa kwa ajili ya mwujiza: Unyakuo wa Kanisa, na kwenda Nyumbani. Kuwatayarisha watu, kuwapunguzia mizigo, kuwaondolea mambo ya ulimwengu, na kuziweka nafsi zao katika Uwepo wa Mungu, ili kwamba Yesu atakapotokea mara ya pili, utukufuni, wale walio tayari watatwaliwa na kunyakuliwa pamoja, kumlaki hewani na kuwa pamoja Naye.

38 "Kama ilivyokuwa katika wakati wa Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwake Mwana wa Adamu; kula, kunywa, kuoa, kuolewa," mambo yote hayo mnayoyaona yakiendelea. Jiweke wazi. . .Mungu akujalie, leo hii, kwamba

ufungue. . .Mungu aufungue ufahamu wako, upate kuona hivi ni vibao vya kuelekeza. Na miujiza ya kimbinguni ikining'inia papa hapa mbele zetu leo hii, ya Kuja Mara ya Pili kwa Bwana Yesu Kristo, nasi tuko kwenye njia panda. Angalieni.

39 Basi Nuhu alipoanza kuwaonya watu, na kuhubiri, wengi wao walimcheka, wakamdhihaki, kwa sababu ujumbe wake ulionekana usio wa kimantiki kabisa.

40 Na siku hizi, watu wangewezaje siku hizi. . .wanaposema, "Tunao madaktari walio bora sana duniani. Tunazo kliniki bora zaidi tulizopata kuwa nazo. Tuna *haya* yote, *yale*, na *mengineyo*. Kwa nini tuhitaji. . . "

41 Sikilizeni. Leo hii, tunahitaji uponyaji wa Kiungu zaidi ya tulivyowahi kuuhitaji. Na kadiri siku zinavyozidi kusonga mbele, zaidi, na zaidi, ndivyo utakavyohitajika zaidi na zaidi. Na itakuwa, baada ya kitambo kidogo, ya kwamba isipokuwa mtu ametiwa muhuri na Roho Mtakatifu, ni vigumu kujua, yeye amejiweka wazi kwa mambo ya kila namna. "Usimkaribie yeyote wa hao walio na Muhuri wa Mungu katika vipaji vya nyuso zao, wakati hayo mapigo makubwa mno yatakapoanza kuanguka." Tuko kwenye njia panda, makutano sasa.

42 Na tunapoona, na kumwona Nuhu, jinsi alivyozungukazunguka, akiwaonya watu, akisema mvua ilikuwa inakuja. Watu hata hawakujua mvua ilimaanisha nini. Haikuwa imewahi kunyesha.

43 Na kuna watu ulimwenguni, siku hizi, baada ya miaka elfu mbili ya kuhubiri Injili, wasiojua maana ya kuzaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu. Hawajui maana ya uweza yote. Ati nini? Mungu katika uweza wa nguvu Zake zote zinazoweza kumbadilisha mtu kutoka kwa mwe—mwenye dhambi wa mitaani, kufikia mahali pa kimalaika katika Ufalme wa Mungu, kama mwana na binti wa Mungu. Hawaelewi. Wamechukuliwa sana, wamelewa vibaya kwa mambo ya ulimwengu. Wanacheza-cheza na ulimwengu, hadharani, wala hawatambui ya kwamba huyo ni pepo mchafu, na ubao mkuu wa kuelekeza uliotiwa alama kwa ajili ya watu wa siku hizi, kutazama na kuwa tayari. Yesu alisema, "Mambo haya yatakapoanza kutokea, inua kichwa chako, ukombozi wako umekaribia."

44 Isitoshe, bali Mungu alionyesha ishara kupitia kwa Henoko, alionyesha ishara kupitia kwa Nuhu, nao ulimwengu ukaicheka. Lakini, siku moja, kulitokea ngurumo na radi. Moto ulikuja kutoka mbinguni. Radi na ngurumo zikaanza kunguruma. Huo ulikuwa ni mwujiza, wenyewe. Ndipo mvua ikaanza kunyesha.

45 Lakini huu hapa ule mwujiza mkuu. Mwujiza ulikuwa ni jinsi ambavyo Mungu alikuwa amemficha mtoto Wake mwaminio kwenye safina ya usalama. Wakati wote ambao ngurumo ilikuwa ikiendelea, mvua ilipokuwa ikinyesha, Nuhu alikuwa anastarehe ndani ya safina pamoja na Mungu,

amekusudiwa kimbele, ameteuliwa tangu zamani, kuingia ndani ya safina hiyo. Wakati hayo mapigo yalipokuwa yakianguka, Nuhu alikuwa katika raha, katika usalama; ambaye alikuwa amechekwa, alikuwa ameingia katika raha.

46 Wale wanaowacheka na kuwadhihaki, siku hizi, kwa sababu mnatamani kuishi maisha ya kujitolea kikamilifu kwa Bwana Yesu, hawatambui kwamba mumefichwa chini ya mikono Yake ya milele. Hawatambui ya kwamba mumetulia kwa usalama tu mwezavyo, katika Mwenyezi, wala hakuna kitu kinachoweza kuwadhuru.

47 Safina ikaanza. . .maji yakaanza kuja, nao watu wakaanza kupiga makelele na kulia, na kupiga mayowe na kuhangaika. Ndipo badala ya safina kuketi pale, ilielea papo hapo juu, wakati wote, ikimbeba Nuhu na kumlaza kitandani wakati ikielea kwenye mawimbi. Hakika. Ilikuwa ni ubao wa kuelekeza. Mungu aliusafisha ulimwengu kabisa, kutokana na dhambi. Alikuwa anataka kuanzisha mpya. Ishara na maajabu yakionekana kabla Yeye hajafanya hivyo.

48 Angalieni, kwenye kule kutoka, wakati Mungu alipowakomboa Israeli, waliokuwa utumwani, kule chini Misri. Kabla Mungu hajaelekeza kidole kimoja kwa Israeli, jambo la kwanza alilofanya lilikuwa ni kufanya ishara ya kimbinguni, kuonyesha kwamba Yeye alikuwa ni Mwenyezi, kwamba alikuwa angali hai. Makuhani na rabi, na kadhalika, wa siku hiyo, walifikiria kwamba Mungu alikuwa hayuko tena, kama tu wanavyofikiria siku hizi. Lakini Mungu angali ni Mwenyezi, Naye angali anafanya mambo ya kimiujiza. Nao walidhani ya kuwa alikuwa hayuko tena. Lakini papo hapo katikati ya wakati huo, Mungu alishuka kwa familia duni na nyenyekevu, ya Lawi, nayo ikamzaa mwana, ambaye alikuwa mkombozi.

49 Na jinsi mtoto huyo Musa alivyokuwa amefichwa ndani ya safina hii. Laiti tungekuwa na wakati wa kuliingilia na kulielezea, jinsi walivyompeleka mtoni kule. Na huko, katikati ya mamba, na chochote kile, akafanya mambo ya kimiujiza.

50 Jinsi alivyomhifadhi Musa, wakati uo huo, jinsi ambavyo walifikiria siku zote za miujiza zimepita. Lakini walikuwa kwenye njia panda. Walikuwa na Neno. Walikuwa na mifupa ya Yusufu. Wote walikuwa sawa. Walikuwa ishara, naam, kwamba Mungu angali hai na anatawala, na alikuwa katika siku moja. Lakini si hayo tu, bali hata hivyo, mbali na Neno, walikuwa na Mungu mweza yote asiyeweza kushindwa, Yule aliye yeye yule jana, leo na hata milele, Yule aliyesimama miongoni mwao wote.

51 Ndipo kwenye umri wa miaka arobaini, wakati Musa alipokuwa amesimama kando ya mto. . .au upande wa jangwa, Mungu alishuka chini katika umbo la Malaika. Naye Mungu, kabla hajaiangamiza Misri, na kuwavuta watoto Wake na

kubadilisha hicho kipindi chote cha wakati, alionekana duniani na kumtuma Malaika kwa masikini na wahitaji. Alifanya ishara na maajabu. Kisha akamwonyesha Musa Utukufu Wake. Jinsi ambavyo angeweza kuchukua fimbo na kufanya muujiza. Jinsi angeweza kuweka mikono yake kifuani mwake na kuuponya, ukoma.

52 Ilikuwa ni nini? Tuna wakati unaobadilika. Tuna makutano ya barabara. Basi yule Mungu mkuu asiyebadilika ambaye alikuwa katika—katika. . .haibadiliki, Yule ambaye alifanya mambo hayo katika njia panda za wakati, uliopita, ni zaidi sana jinsi gani Yeye atafanya sasa wakati kuzimu yote imeshikwa na hamaki na wakati wa mwisho umewadia! Yeye ni yule yule. Hashindwi. Mwenyezi anakutana na mambo ya kimiujiza. Hakika. Yasiyotafutika. . .Mawazo ya mwanadamu yasiyo na busara hayawezi kamwe kuyafahamu mambo ya kimiujiza. Inabidi uwasiliane na Mwenyezi. Halafu basi unapofanya hivyo, unawasiliana na mambo ya Kimbinguni. Maisha yako yanabadilika, mawazo yako yanabadilika, akili zako zinabadilika. Unafanywa tofauti. Magonjwa yako yanatoweka. Nguvu kuu za Mungu zinaingia ndani.

53 Musa, kwenye kile kichaka. Yeye alimwona na kumsikia Mwenyezi, naye akaona ya kimiujiza. Mungu hakuridhika na kumpa Musa ujumbe tu, kushuka kwenda na kuhubiri, peke yake, kwa Wamisri, na kuwahubiria Waisraeli. Mungu, Mwenyezi na Mungu wa miujiza, hakuwa Mu—Mungu tu wa kulifunulia tu mtu mmoja. Lakini alisema, "Chukua ishara hizi!" Haleluya! "Chukua ishara hizi na ukazionyeshe huko chini. Nitakuwa pamoja nawe."

54 Badiliko! Njia panda ilikuwa imewadia; wakati wa jambo fulani kutukia. Lakini kabla jambo hilo halijatukia, Mungu hutoa onyo Lake. "Mimi ningali Yehova. Ningali hai. Nami ni mwenyezi. Nami ndimi Mungu wa miujiza."

55 Naye wakati akishuka Misri, alichukua fimbo yake na kuitupa chini, naye akauponya mkono wake wenye ukoma, na kufanya mambo hayo.

56 Ndipo ninawatakeni muone, kila wakati mambo ya kimiujiza yalipofanywa, Shetani sikuzote yuko hapo kuyaigiza. Na vile alivyokuwa akiiga siku hiyo, angali ni mwigaji yule yule siku hizi. Hata maigo yake yanaelekeza tu kwenye wakati wa mwisho kwenye njia panda.

57 Walikuwa na baadhi ya maskini wapiga ramli wa kale, na kule chini, walioitwa Yane na Yambre, ambao walisimama. Nao wangeweza kutupa fimbo zao chini na kuzigeuza kuwa nyoka, na kadhalika, na kufanya tu kama yeye alivyofanya, walifanya. Lakini Mungu alithibitisha ni nani alikuwa Mungu. Wangeweza kuleta mapigo, lakini wasingeweza kufanya uponyaji wa Kiungu, maana ni Mungu pekee anayeweza kuponya. Nao

wangeweza kuleta jipu, lakini wasingeweza kuliondoa. Mungu alisimama katika Nguvu Zake pale, kuonyesha ya kwamba uponyaji halisi wa Kiungu ulikuwa ndio mambo Yake ya kimiujiza, kuthibitisha Mwenyezi kwenye njia panda.

58 Wamisri waliitisha majipu, lakini yakawatokea wenyewe. Lakini mtumishi wa Mungu angeweza kuyaondoa. Kwa nini? Wanaweza kuiga.

59 Tunafundishwa, katika siku hizi za mwisho, ya kwamba kungekuwa na kitu kile kile. "Kama vile Yane na Yambre walivyoshindana na Musa, vivyo hivyo hawa nao wataikataa ile Kweli; watu walioharibikiwa akili zao, katika habari za imani." Jinsi ambavyo wangefanya! "Wakaidi, wenye kujivuna; wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wasiotaka kufanya suluhu, wasiotosheka. Wenye mfano wa utauwa."

60 Loo, jinsi ambavyo siku tunazoishi, makutano ya barabara; mwishoni mwa safari, mwishoni mwa wakati! Mungu anathibitisha. Ni siku ya ajabu jinsi gani kuishi.

61 Mungu aliwathibitishia, na kujithibitisha Mwenyewe, na kupata utukufu. Jinsi alivyoshuka huko Misri na kulipiga taifa hilo! Jinsi alivyowatoa Israeli juu ya mbawa za tai, na kufanya ishara na maajabu, kwa maana Yeye ndiye Mwenyezi wetu. Naye hufanya mambo ya kimiujiza.

62 Kabla hajazamisha magari ya farasi ya Farao, alitoa kila namna ya ishara. Alitoa ishara za uponyaji wa Kiungu. Alitoa ishara na uthibitisho wote wa uweza Wake. Jinsi angeweza kumwokoa mwana mkubwa, ama kumchukua mwana mkubwa. Jinsi angeweza kuharibu, au jinsi angeweza kuokoa maisha. Jinsi angeweza kufanya miujiza. Angeweza kufanya mambo ya miujiza. Na jinsi jua na mwezi viligeuka kuwa giza! Jinsi mvua ya mawe ilivyoikumba nchi. Jinsi radi ilivyoenea nchini na kuwaua ng'ombe, na kadhalika, kama tu ilivyofanya katika siku za Nuhu.

63 Naye akasema, "Katika siku za mwisho, mwezi utashindwa kutoa nuru yake, wala jua halitaangaza. Nalo litakuwa jeusi kama gunia; litiririke kama damu," litakapouficha uso wake na kulia, lenyewe, na kutokwa jasho na matone yaliyojaa damu ya huzuni. Mungu atakuwa duniani, Mwenyezi, akifanya mambo ya kimiujiza. Bila shaka. Anaweza. Yeye ni mweza yote. Wazieni jambo hilo.

64 Huko, huko chini Misri, jinsi alivyofanya hizo ishara na maajabu, na mambo ambayo alikuwa amefanya! Yeye ni Mungu. Hakuna awezaye kupachukua mahali Pake.

65 Angalieni, Mungu alifanya mwujiza Wake, kisha akampa Farao nafasi. Naye Farao akashindwa na akakataa kuchukua nafasi yake. Hakuna kitu kilichosalia.

66 Mtu anapoikataa rehema ya Mungu, kuna kitu kimoja tu kilichosalia, hicho ni hukumu. Na, rafiki yangu mpendwa, leo hii, Mungu akitusaidia, unapoona mwisho wa somo hili ukija, nawe uikatae rehema uliyopewa na Yesu Kristo, Roho Mtakatifu, hakuna kitakachosalia ila hukumu ya Kiungu. Hakuwezi kuwa na chochote kilichobaki.

67 Hatimaye Farao alitenda dhambi akamalizia siku yake ya neema wala hapakuwapo na kitu kilichosalia, maana njia panda ilikuwa imekaribia. Naye Mungu akauwekea wakati njia panda.

68 Wakati Lutu na Ibrahimu, wakati mwingine, wakati Ibrahimu alipokuwa awe mtawala wa ulimwengu, uzao wake ulikuwa utawanyike juu ya nchi. Alikuwa pamoja na mpwake Lutu, ambaye alikuwa ni jamaa.

69 Na ni picha nzuri jinsi gani leo hii ya kanisa baridi, la kawaida lisilojali; kwa Kanisa la Mungu aliye hai lililozaliwa kwa Roho, lililoteuliwa, lililoitwa litoke, lililotengwa. Wanaishi pamoja kwenye uwanda mmoja.

70 Lakini hatimaye ulifika wakati ambapo Lutu alilitwaa kundi lake kuu na kushuka kwenda Sodoma na Gomora, ambapo wangekuwa maarufu, ambapo wangechukua nchi iliyo bora sana. Naye Ibrahimu akakaa katika mapenzi ya Mungu na kuchukua nchi kame. Sara, mke wake mrembo, na Ibrahimu, walikaa juu ya nchi kame, kusudi waweze kumtumikia Bwana.

71 Mungu haahidi maisha rahisi. Usimpotoshe Mkristo. Wala usiupotoshe Ujumbe, kwa kuwaambia, kwamba, "Kila kitu kitakuwa sawa. Hakuna kitakachokudhuru. Hakuna kitakachodhuru. Hakuna majaribu wala chochote kile." Huo ni uwongo.

72 Kama mshairi alivyosema, "Ni lazima nibebwe kwenda Mbinguni kwenye kitanda cha raha, huku wengine walipiga vita kushinda tuzo na kuabiri bahari zilizojaa damu?" La, bwana.

73 Mungu haahidi urahisi na mafanikio. Lakini anaahidi neema, kuvumilia katika kila wakati. Neema ndiyo tunayotazamia.

74 Ibrahimu alichagua njia ya Mungu. Alikaa juu ya kilele cha mlima, huko hakukuwako na nyasi nyingi kwa ng'ombe wake. Lakini, Lutu, mfano wa ulimwengu uliorudi nyuma, kanisa ambalo haliamini katika mambo ya kimiujiza. Ndipo hatimaye ikafikia ambapo mambo hayo yalimfikia Mungu, hata ikabidi ije njia panda. Ilibidi kuwe na wakati. Kwa maana, Ibrahimu alikuwa ndiye mrithi wa nchi.

75 Ee Mungu, kwa nini Wakristo hawawezi kuona? "Heri wenye moyo safi; watamwona Mungu. Heri wenye upole; watairithi nchi." Wakati wa njia panda umekaribia; Baba yetu kuonyesha kwamba tuko kwenye wakati wa mwisho. Mnaona? Mambo ya

kimiujiza, mambo ya kimbinguni, Mwenyezi akifanya mambo ya kimiujiza. Mwangalieni.

76 Kama vile katika wakati wa Ibrahimu, kabla tu ya wakati wa mwisho, angalieni kile kilichotukia ulimwenguni, huko chini Sodoma, katika jiji kubwa.

77 Ibrahimu aliishi katika hema, ambaye alikuwa mrithi wa vitu vyote, aliishi katika hema. Kwa hivyo si ajabu mshairi angeweza kusema, "Hema au kibanda, kwa nini nijali?" Wewe ni mrithi wa vitu vyote, ikiwa uko ndani ya Kristo. Mungu amempa dunia, Naye ndiye Mfalme. Nasi tuko ndani Yake, mrithi wa vitu vyote, mweza yote, mtenda miujiza, na kwenye njia panda ya wakati.

78 Angalieni kwa makini sasa, tunapoendelea katika hili. Angalieni jinsi Mungu alivyofanya kabla tu ya wakati wa mwisho.

79 Lutu, kule chini Sodoma. Upotovu ulikuwa unaongezeka. Wanaume wakawa mashoga, wapotovu, wakibadilisha mfululizo wa maumbile asili ya mwanadamu na kuupotosha.

80 Angalieni ulimwengu siku hizi. Kitu hicho chote kinakuwa ni kipindi cha wakati uliopotoshwa. Na mahali pazuri sana, ambapo watu huenda kusomea dini, katika shule kuu. Nami nimelizungumzia hilo na kulifahamu, ambapo wanaume hawaruhusiwi kuoa wanawake, lakini linachukiza sana. Na jinsi ambavyo shuleni siku hizi, katika makanisa haya ya kisasa huko nje, jinsi jambo hili kuu! Wanaume wamekunywa pombe na kuvuta sigara, na kuchochea uchu, na kuwaharibu wasichana wadogo na kadhalika, nao walianza katika uchanga wao, mpaka mfululizo wao halisi wa maisha umepotoshwa. Mungu amewaachia uharibifu. Nayo maisha yao yamechanganyishwa sana hata wao si wanaume na wanawake wa asili tena. Ibilisi amewakamata sana.

81 Angalieni njia panda kule pamoja na Sodoma na Gomora. Angalieni njia panda katika siku za Nuhu, kuoa na kuolewa. Mnauona huo ubao wa kuelekeza? Ilikuwaje? Wakati uo huo, Mungu alikuwa na nabii duniani.

82 Kabla ya wakati wa mwisho. . .Hili hapa. Sikilizeni! Sikuzote, kabla ya wakati wa mwisho, wakati Shetani anapowaachilia waigaji wake, Mungu huwatuma manabii Wake. Nasi tunaambiwa katika Biblia, kwamba, "Katika siku za mwisho vijana wenu wataona maono, na juu ya watumishi Wangu wanawake na wanaume."

Manabii watatokea tena duniani. Waona maono watatokea duniani, katika wakati wa mwisho. Tuko hapa. Tuko kwenye njia panda. Imetabiriwa na manabii wote watakatifu, kote katika wakati, na kutabiriwa na Neno takatifu la Mungu. Wakati wa mwisho: jinsi Bwana atakavyofanya, jinsi baraka

Zake zitakavyokuwa, na kile ibilisi atakachofanya katika siku hizo, kile kitakachotukia, wakati wa mwisho.

83 Utakatifu wa Mungu hauwezi kustahimili uovu wa ulimwengu. Lakini kabla hajaufikisha kwenye njia panda, anatuma miale myekundu ya maonyo. Si hayo tu, bali kabla Mungu hajaiharibu Sodoma na Gomora, Yeye pia aliwatuma Malaika duniani, ambao walijichanganyisha miongoni mwa wanadamu.

84 Na kabla ya wakati wa mwisho, Mungu aliahidi atawatuma Malaika. Nasi tunawaona. Wanakuja na Jumbe za mwenyezi Mungu. Wakati wa njia panda! Si zaidi ya majuma matatu yaliyopita, kumwona yule Mwenye nguvu amesimama pale, Yeye aliyesimama tangu nilipokuwa mvulana mdogo, na kuzungumza. Mimi si mlokole; mnajua hilo. Lakini ni kuyatimiza Maandiko.

85 Nafikiri kanisa hili linapaswa kujua Kweli, na ishara ya mahali tulipo; msije mkawa wavivu; mpate kuwa watenda kazi hodari; tofauti hizo zipate kutatuliwa, nanyi mtatembea kama wanaume na wanawake watauwa, huku moyo wako umewekwa juu ya Kristo. Wala usiangalie mambo haya ya uwongo ya dunia, maana ni ya ibilisi; ugomvi huu wote na vita, na mizozano na tofauti. Usiyaangalie. Tuko mwisho. Pia, kumbuka, huenda usiwe na juma lingine la kulifanyia. Sijui. Mungu pekee ndiye ajuaye. Tuko hapa kwenye mwisho.

Kulikuwako na Nuhu, katika wakati wake.

Hawa hapa Israeli, katika wakati wao.

86 Huyu hapa Ibrahimu, kwenye njia panda nyingine, kati ya (u—ulimwengu) mambo ya asili na ya kimbinguni. Malaika walishuka. Walionekana kama wanadamu. Utukufu! Nao wakasimama karibu na Ibrahimu, nabii, na kumwambia, "Ibrahimu, Mungu atafanya mambo ya kimbinguni. Yapata wakati huu, mwaka ujao, kwa muhula wake, nitakurudia. Mke wako, mwenye umri wa miaka mia moja, nanyi mtamzaa mtoto. Nitakuonyesha nguvu Zangu, uponyaji wa Kiungu. Nitakubadilisha, na kukurudisha kuwa kijana tena. Nami nitambadilisha Sara, na kumfanya mtu tofauti." Atamfanya msichana. "Mimi ni wa kimiujiza. Mimi ni mwenye nguvu zote. Mimi hufanya mambo ya kimiujiza. Amina. Nitakuonyesha nguvu Zangu. Ibrahimu, tuko kwenye wakati wa njia panda. Pepo wachafu wako kule chini Sodoma. Naam. Wanafanya kazi miongoni mwa walimwengu huko chini."

87 Wanafanya kazi hapa leo. Mipepesuko, na madoido, na kufanya mizaha michafu, na mambo haya yote machafu kwenye redio, televisheni, hata hayakaguliwi wala chochote kile. Na kupotosha, wakati mwingine, Injili, kuwa jambo la kijamii. Ulimwengu mzima umepotoka. Lakini wakati uo huo ulimwengu umepotoka, waaminio wameongoka, wakamjia

Bwana na Nguvu za Mungu, kwa kufanya kazi na kuonekana kwa Mwenyezi. Jinsi ambavyo Mungu, katika rehema Zake, anaonyesha mambo haya!

88 Kasema, "Ibrahimu," wakati nabii huyu akiketi chini ya hema lake, mzee, huko juu katika nchi kame. Alijali nini? Hema, au kibanda, ama kibanda, nini, haikuleta tofauti yoyote kwake. Alikuwa mrithi wa hayo yote. Kila kitu kilikuwa ni mali yake, naye alijua.

89 Vivyo hivyo mwaminio anajua leo hii. Je, tunajali nini kuhusu mambo haya ya duniani? Hiyo ndiyo sababu niliiacha ile mikutano, si muda mrefu uliopita, kwa sababu nisingeweza kuwafinyilia watu watoe matoleo. Sijali watu wanasema nini, ninaamini kwamba Mungu ni mkubwa vya kutosha kujazi kila kitu anachohitaji. Naam, bwana. Afadhali nile biskuti za magadi na kunywa maji ya chumvi, na kuhubiri Injili, kuliko kuwa na mambo mazuri ya ulimwengu. Haijalishi, ikiwa tutawafanya kujikabidhi wenyewe mikononi Mwake, na kumtazamia Mwenyezi. Hiyo ni kweli.

90 Tazama mahali lilipo. Nasi tunamwona anapofuata, huku Ibrahimu ameketi chini ya hema lake, nao Malaika hawa wakamtokea.

91 Wameshuka kwenda Sodoma na Gomora. Nasi tunaona ya kwamba Mungu, katika siku hiyo, alifanya miujiza. Alishusha moto kutoka mbinguni na kuufagilia mbali huo mji, na kuitakasa nchi, na kuikabidhi yote kwa Ibrahimu. Naye mke wa Lutu akageuka kuwa nguzo ya chumvi, kwa sababu alitazama nyuma, kama ukumbusho wa fedheha; ambaye alikuwa mwanamke mashuhuri miongoni mwa jamii za jiji hilo, la Gomora na Sodoma. Na mabonde yote yaliangamizwa, wakati Mungu alipofanya mambo ya kimiujiza kwa moto na kiberiti kutoka mbinguni.

92 Ni wakati mzuri jinsi gani! Ni wakati mzuri jinsi gani wa kuishi! Mungu, katika nguvu Zake! Ikaja njia panda tena. (Nafikiri ninabanwa na wakati, itabidi niharakishe.) Anakuja Mweza yote, ule Uwepo tena.

93 Kulikuwa na jamaa aliyeitwa Ahabu, aliyemwoa msichana aliyeitwa Yezebeli. Ambaye, alikuwa mwaminio hapo mwanzoni, Ahabu, aliyezaliwa Myahudi, akatahiriwa siku ya nane, kulingana na torati. Naye alilelewa katika nyumba ya kidini, kumwamini Yehova, lakini akapendana na maskini kipusa mwenye macho ya kuvutia ya mwabudu sanamu. Hiyo ni kweli.

94 Na, suku hizi, wanaume wazuri Wakristo walianguka chini ya ushawishi wa upuuzi kama huo na madoido, kwa sababu moyo huo haujawa thabiti katika Kristo Yesu. Naam. Ni siku ya jinsi gani tunayoishi, ni wakati wa jinsi gani, vibao vya kuelekeza vinaangalia hapa juu usoni.

95 Lakini, basi, kabla tu Mungu hajaleta shindano la kuamua, kuonyesha ni nani alikuwa Mungu, ulifika wakati ambapo kulikuwa na nabii aliyekuja nchini, jina lake Eliya, ambaye alitiwa mafuta na ujumbe wa Mungu. Naye akafanya mambo ya kimiujiza na kuthibitisha kwamba Mwenyezi alikuwa angali ni wa kimiujiza. Nabii alisimama pale na kuzifunga mbingu, hata haikunyesha katika siku za huduma yake. Naye akashusha mvua kutoka mbinguni na kuipa dunia. Nao Malaika wakatokea jukwaani, haleluya, wakamwokea mikate kadhaa ya nafaka ambayo ilimdumisha akiwa hai, siku arobaini, alipokuwa huko nje nyikani pamoja na Mungu.

96 Malaika wanaonekana katika wakati wa mwisho. Manabii wote na vibao vya kuelekeza vinaonyesha, katika siku hii, kwamba malaika watatokea, manabii watatokea, ishara na maajabu. Na kama Mungu alifanya hivyo kwa ajili ya hizo njia panda ndogo kule nyuma, atafanya nini sasa wakati kuzimu yote imefunguliwa? Mbingu yote itafunguliwa, malaika wakitokea, ishara na maajabu duniani. Mambo ya bandia yanaibuka. Mungu akithibitisha ni lipi sahihi na lisilo sahihi. Amina.

97 Loo, ninampenda Yeye! Nina hakika mnampenda, pia. Simaanishi kuwapigia kelele, lakini inawaka nafsini mwangu, nikiwazia, jinsi ambavyo katika siku hii.

98 Kabla tu hajawakomboa, Yeye alifanya ishara na maajabu ya kila namna. Walituma kundi la watu kule, kumchukua nabii huyu kwa nguvu. Akasema, "Ikiwa mimi ni mtu wa Mungu, moto na ushuke kutoka mbinguni."

99 Angalieni jinsi moto unavyokuja kila wakati. Angalieni jinsi manabii wanavyokuja kila wakati. Angalieni jinsi mambo ya kimiujiza yanavyofanyika kila wakati. Tazama jinsi Mungu anavyojithibitisha Mwenyewe katika uponyaji na nguvu kila wakati, kwenye njia panda tu, kamwe si kabla; papo hapo kwenye njia panda, kwenye makutano, mabadiliko katika vipindi vya wakati, mabadiliko ya wakati.

100 Sasa, kwa mafungu machache ya kumalizia, angalieni kwa dakika moja. Tutaenda sasa kwe—kwenye njia panda kuu ya tano, moja ya njia panda kuu, maana ya tano ni *tano*, Y-e-s-u. [Kiingereza: J-e-s-u-s.—Mfa.] Amina. Unakuja wakati ambapo swali la dhambi lilipaswa kutatuliwa. Unakuja wakati ambapo yule wa kimiujiza hana budi kujifanya Mwenyewe aeleweke kikamilifu. Unakuja wakati ambapo mioyo ya watu ilibidi ibadilishwe, maana torati na waamuzi, na kadhalika, hawawezi kufanya hivyo. Damu ya mafahali na mbuzi haikuweza kuiondoa.

101 Na kabla tu ya ile njia panda kuu kuja, ibilisi alitokea miongoni mwa wahubiri, kasema, "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama hicho."

102 Na, wakati uo huo, Mungu akatuma Malaika duniani. Kulikuwa na mzee huko chini ambaye alikuwa ameweka nyumba yake katika utaratibu, jina lake Zakaria. Alikuwa anaomba. Siku moja alipokuwa madhabahuni, akitikisa uvumba wake, akiwaombea watu, kukatokea upande wake wa kuume, Malaika mkuu, ikithibitisha ya kwamba wakati wa njia panda ulikuwa umekaribia. Akamwambia kwamba angemzaa mvulana, kutoka kwa mke wake, ambaye alikuwa amezeeka na mwenye umri mkubwa. Na jina lake lingekuwa Yohana.

103 Yohana akatokea, akidai mambo ya kimiujiza. Yohana alikuwa nabii. Biblia ilisema, Yesu alisema, Mwenyewe, "Hapajapata kuzaliwa mtu kama yeye duniani," kufikia wakati huo. Haleluya! Kwa nini? Yeye alikuwa nabii, aliye mkuu kuliko wote waliokuwako kufikia wakati huo. Kwa sababu, hii ilikuwa ndiyo njia panda kubwa sana ambayo Mungu aliwahi kufanya na ibilisi, wakati njia zao zilipokutana, na hapo angemvua na kumnyang'anya kila kitu alichokuwa nacho. Haleluya! Yohana alikuwa ni nabii.

104 Gabrieli alikuwa ndiye Malaika pale, akitokea wakati wa njia panda. Utukufu kwa Mungu! Yapata miaka thelathini na mitatu kabla halijatokea, Mungu alianza mapema sana, kutangulia kuwaonya ya kwamba wakati wa njia panda ulikuwa umekaribia. Wasioamini wakazidi kuzoroteka, na kulizamisha, na kulizozania, na kujaribu kupita nayo. Kisha, hatimaye, wakaua kila mtu waliyemtuma, na kadhalika. Lakini Mungu akaendelea katika mambo ya kimiujiza, vivyo hivyo tu, kwa kuwa Yeye ni mweza yote. Hana budi kuwa hivyo. Yeye ni Mungu.

105 Angalieni kilichotukia sasa, tunaposonga mbele katika kisa hiki—hiki hapa. Tunapopanda, tunamwona Yohana akija mtoni, akihubiri. Anazungumza juu ya Mtu ambaye anakuja, ana nguvu kuliko yeye; akaanza kuhubiri. Baada ya kitambo kidogo, alionekana si mwingine ila Mwenyezi Mwenyewe, akiwa amefunikwa na fungu dogo la nyama. Yehova Mungu Mkuu akajifunua Mwenyewe katika Mwanawe, Kristo Yesu. Mwenyezi akafanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, akatembea miongoni mwetu. Haleluya!

106 Alipokuwa akitembea juu ya Bahari ya Galilaya, usiku mmoja, amelala kule, ile mashua ndogo ya kale ikiyumbayumba huku na huku, alijifanya kana kwamba hata hakujali. Alikuwa amechoka. Lakini ukafikia wakati wa njia panda; ilibidi jambo fulani litukie. Akaweka mguu Wake kwenye demani ya mashua, akaangalia juu na kusema, "Amani. Tulia." Ninawaambia, Muumba mwenyewe wa mbingu na nchi alilala katika mashua hiyo, na ilibidi maumbile kumtii. Mweza yote anapozungumza, mambo ya kimiujiza hufanyika. Amina.

107 Mwenye ukoma aliyejaa ukoma, alimwendea siku moja, kasema, “Bwana, unaweza ukipenda, unaweza kunitakasa.”

108 Akamgusa, akasema, “Nataka. Takasika.” Na wakati Mweza yote anapozungumza, mambo ya kimiujiza hufanyika. Haleluya! Ukoma wake ukatoweka, kama jua linavyoruka kutoka nyuma ya wingu. Hakika. Mweza yote hunena.

109 Aliahidi, katika siku hizi za mwisho, ya kwamba angenena tena. Mweza yote anapozungumza, mambo ya kimiujiza hutokea. Naam, bwana.

110 Angalieni. Yeye aliwaponya wagonjwa. Akawafufua wafu. Akafumbua macho ya vipofu. Ilikuwa ni nini? Kuwathibitishia watu kwamba njia panda imewadia. “Ninao Uweza wa kuuweka chini uhai Wangu. Ninao Uweza wa kuutwaa tena. Hakuna mtu aniondoleaye.”

111 Siku moja, katika Yohana 17, aliangalia juu na kusema, “Baba, saa imekwisha kufika.” Haleluya! “Njia panda iko hapa. Mambo yote yamekwisha sasa. Mambo yote yanajiweka tayari. Njia panda zimekuja. Dunia imeonywa. Nimewatia mafuta mitume hawa, nao wamefanya ishara na maajabu. Tumepitia nchini. Tumeichambua huku na huku. Wakati umewadia. Wakati umewadia.”

112 Ndugu, kama mhubiri wa Injili asubuhi ya leo, ninaamini ya kwamba Roho Mtakatifu, akizungumza kupitia midomo ya mwanadamu leo hii, ya wahudumu waliotiwa mafuta, wanazungumza, “Wakati umefika.” Wakati umewadia, na Mweza yote anajibu. Mambo ya miujiza yanafanyika; hayana budi; tuko kwenye njia panda.

113 Na, pale, wakati Yeye alipofanya mambo yote ya kimiujiza, huku Mweza yote, Mungu amedhihirishwa katika mwili.

114 “Nena neno, Bwana, na mtumishi wangu atapona. Mtumishi wangu atakuwa. . .Ataishi.” Alijua. Akida yule wa Kirumi alijua. Alikuwa mtu aliye chini ya mamlaka, hata alijua ya kwamba chochote kilichokuwa chini yake kilikuwa. . .Lolote alilosema, iliwabidi kulifanya. Alisema, “Ninamwambia huyu, ‘Njoo,’ na anakuja. Na mtu yule, ‘Nenda,’ anaenda.” Kasema, “Mimi ni mtu niliye chini ya mamlaka. Na kila kitu kilicho chini ya mamlaka yangu hunitii. Na, Bwana, sistahili Wewe uje nyumbani mwangu. Sema tu neno.” Haleluya! Alijua, huyo alikuwa ni Mweza yote. Alijua wakati Mweza yote aliponena, miujiza ingetendeka. Loo, jamani!

115 Hapo alisimama kwenye kaburi la Lazaro, akilia, kama mwanadamu katika mwili wake. Martha akasema, “Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa. Lakini hata sasa, Mweza yote, nena! Lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atalifanya. Lolote utakalosema, Yeye atalifanya.” Huko, akatembea mpaka kaburini.

116 Mweza yote, akidhihirishwa hapa miongoni mwetu, akiishi pamoja nasi. “Mungu, ndani ya Kristo, aliupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.” Hapa aliishi pamoja nasi, Mungu akijithibitisha Mwenyewe kupitia Mwanawe, Kristo Yesu. Alikuwa mweza yote na wa kimiujiza.

117 Na kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele; Naye alisema, “Sitawaacha kamwe. Kamwe sitawapungukia. Nitakuwa pamoja nanyi hata mwisho wa dunia.” Tunawezaje kutazamia kitu kingine chochote isipokuwa, anapozungumza, miujiza itendeke? Tunawezaje kutarajia kitu kingine chochote?

118 Kwa hiyo Huyu hapa anaenda, chini kaburini, akilia. Ndipo Mweza yote akajikusanya Mwenyewe pamoja, Naye akanena. “Lazaro, njoo huku!” Na mtu ambaye tayari alikuwa akioza; pua yake ilikuwa imeanguka kutoka usoni mwake, katika siku nne. Mabuu ya ngozi yalikuwa yemeshaingia. Uharibifu ulimjua Bwana wake. Haleluya! Akaurudisha uhai wa mtu huyu aliyekufa. Ndipo mtu aliyekuwa amekufa, akasimama kwa miguu yake akaishi tena. Mambo ya kimiujiza!

119 “Mimi ndimi huo ufufuo na Uzima,” asema Mungu. “Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Na kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe.”

120 Ongea, Mweza yote! Mambo ya kimiujiza yatatukia. Naye sikuzote hufanya hivyo kwenye njia panda. Nasi tuko kwenye njia panda. Mtahadhari mnapoona mambo haya yakitendeka. Tuko kwenye wakati wa mwisho.

121 Mweza yote anazungumza, na mtu aliyekufa, maiti, akaishi tena; akasimama kwa miguu yake, na akaenda kwenye dhifa na kula chakula cha jioni pamoja Naye. Loo, jamani! Nini kilitokea?

122 Siku moja tukufu! Sisi sote ambao wakati mmoja tulikuwa tumekufa katika dhambi na makosa; Mweza yote alizungumza. Tulikuwa tunaenda kuzimu, ndipo Mweza yote akazungumza. Tumefufuka kutoka kuzimu, kuingia Utukufuni, na siku moja tutakula Karamu ya jioni katika siku ya mwisho. Mweza yote hunena. Neno la Mungu lina nguvu zote. Tunaliamini, na tukafufuka kutoka mautini kuingia Uzimani.

123 “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kuniamini Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe.” Mweza yote!

124 Sisi ni kama Nuhu, tukijenga safina. Ya kimiujiza yatatokea siku moja wakati Unyakuo utakapokuja na Yesu aje. Tuko kwenye njia panda sasa. Mtakapoona mambo haya yakitukia, inueni kichwa chenu, ukombozi wenu unakaribia. Mweza yote hunena na mambo ya kimiujiza yanafanyika.

125 Kasema, “Tuko kwenye njia panda, Baba. Sina budi kuthibitisha Wewe ni Nani.” Naye akawafufua wafu. Akawaponya wagonjwa.

126 Hatimaye saa Yake ya kuondoka ilipowadia, alitembea kwa unyenyekevu hadi msalabani na akatundikwa pale, akatandazwa. Hakuwa wa Mbinguni; alikataliwa Mbinguni. Akakataliwa duniani. Baada ya watu kuona ishara na maajabu aliyofanya, walimdhihaki na kumcheka; ulimwengu huu mwovu wa dhambi. Lakini wakati ile hukumu ilipomwinua, ilipoiinua ile safina, ile hukumu ya maji; vivyo hivyo na Yesu, huku hukumu ya Mungu ikimiminwa juu Yake. Alikufa badala yetu, na akainuliwa juu.

127 Naye mwaminio anatulia ndani Yake, kama vile Nuhu katika safina. Acha hukumu ipite, inaleta tofauti gani? Hakika. Ati nini? Ati nini? Hata mauti yenyewe hayana vikwazo, hayana uchungu. "Ewe mauti, u wapi uchungu wako? Kaburi, u wapi ushindi wako?" Hainitishi kupitia makaburini. Ninaweza kupiga makelele ya sifa za Mungu, kwa maana najua, na kuwa hai ndani Yake hata milele. Bila shaka.

128 Mweza yote amenena. Alinena na moyo wangu. Alinena na moyo wako, ya kimiujiza yakafanyika. Wakati mmoja maskini mwenye dhambi mwoga, labda. . . kama ulivyofanya, mlevi, au mvuta sigara, ama mkimbia kwenye madansi na mambo ya kipuuzi namna hiyo. Mweza yote alinena, nawe ukalipokea, nayo ya kimiujiza yakafanyika; nawe ukabadilika kutoka mautini kuingia Uzimani, na kuacha dhambi zako! . . .?. . . Mweza yote akazungumza, na ya kimiujiza yakafanyika. Hakika.

129 Kunao watu wanaoketi katika kanisa hili, asubuhi ya leo, miaka michache iliyopita walikuwa wamefungwa na kansa, wakifa. Kuna wale ambao wameketi hapa, waliokuwa vilema na wasiojiweza, na viwete na waliopooza. Ndipo Mweza yote akanena, nayo ya kimiujiza yakafanyika. Bila shaka. Hakika. Ishara ni nini? Tuko kwenye njia panda. Tuko kwenye njia panda sasa. Tunajiandaa kuingia kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu.

130 Sasa angalieni, tulipanda juu. Nao walipofanya hivyo, walipomtandaza kati ya mbingu na nchi, Mbingu hazingeweza kumpokea, dhambi ya ulimwengu zilikuwa juu Yake. Nao ulimwengu ukamkataa, kama Mfalme wao. Hapakuwa na mahali palipoachwa kwa ajili Yake kufia. Asingeweza kuja Mbinguni, kwa maana alikuwa amebeba dhambi za ulimwengu. Alichukiwa na kudharauliwa, na kutemewa mate, na kukataliwa na kutupwa na dunia. Lakini alisimama kati ya mbingu na nchi, na akaiunganisha njia. Na kila mwanamume ama mwanamke anayetaka, anaweza kuja kupitia mkondo huo wa Damu kutoka ubavuni Mwake, kuingia Utukufuni. Mwenyezi!

131 Nini kilitokea? Ishara na maajabu yalifanyika. Ilikuwaje? Mwezi ukaanza kulia. Jua likafunga macho yake likaanza kulia. Nalo likaingia katika dhiki kubwa sana, hata likawa na msukosuko, ikawa kama damu inayotiririka. Hakika, lilifanya hivyo. Walipomwona Muumba wa mbingu na nchi,

amekataliwa na dunia. Na, dhambi nyingi sana, asingeweza kuingia Mbinguni; na akifa kama mpatanishi kati ya Mungu na mwanadamu, amesimama kati ya mbingu na nchi.

132 Jua lisingeweza kustahimili, likasema, "Sitaangaza tena," kwa hiyo likaingia giza. Nyota zikasema, "Siwezi kuangalia hili." Naam. Ardhi ikasema, "Siwezi kuvumilia," nayo ikashikwa na mavune ya fadhaa, na kububujisha miamba kutoka ardhini. Ya kimiujiza yakafanyika! Ulikuwa ni wakati wa mabadiliko, ulikuwa mwisho wa safari, dhambi ilikuwa imetawala, mpaka kwa msalaba, lakini dhambi ililipiwa hapo. Loo, jamani! Ndipo nchi ikatikisika sana mpaka ikatupa mawe kutoka ardhini mwake, ama ikayaning'inizia vilimani. Hata ilitetemeka sana mpaka wafu wakafufuka kutoka kaburini. Nena kuhusu mavune ya fadhaa! Ndipo jua likaanza kushikwa na misukosuko, nalo likatoka. Ya kimiujiza yakafanyika! Haleluya! Sikuzote hufanyika kwenye njia panda.

133 Angalieni kilichofanyika hapo, na hicho kilikuwa tu kikijiandaa kwa ajili ya jambo hili. Wakaingia katika nyakati za giza, miaka elfu moja na mia tano. (Laiti tungalikuwa na wakati, lakini tumebanwa. Ninataka kuondoka saa sita.) Basi angalieni, hilo, likija kupitia pale na zile nyakati za giza. Laiti tungalikuwa na wakati wa kuingia katika ule wakati, yaliyotukia katika wakati wa Wesley na Luther, mara hiyo ya sita, kwamba kulikuwa na badiliko lililoingia, wakati kanisa lilipowekwa huru kutoka gizani nalo likaletwa katika nuru ya ajabu ya Injili tena. Ishara na maajabu! Ee Mungu, jinsi hakuna mtu aliyesimama, huku uponyaji wa Kiungu na ishara na maajabu yakatukia. Na ilikuwa ni kati ya dhabihu na kule Kuja mara ya Pili, basi hebu angalieni yaliyotukia wakati huo. Wakati John Wesley alipohubiri Injili, alifukuzwa makanisani na kadhalika, mpaka watu wakaanguka sakafuni, wakawamwagia maji usoni. Hawakujua walikuwa na shida gani, wakizimia chini ya Nguvu za Roho Mtakatifu. Ishara, na maajabu, na miujiza, na uponyaji, vilifanyika.

134 Sasa, ndugu, dada, sikilizeni. Ni nini kinachofanyika sasa? Tuko kwenye wakati wa mwisho. Tunaingia kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu; kila mkono ukielekeza huko. Maskini ile saa ya kale inapiga, yapata dakika mbili ifike usiku wa manane. Mweza yote anazungumza. Malaika wanatokea. Manabii wanakuja. Manabii wanatabiri. Maono yanamiminwa juu ya watu hao wa siku hizi. Injili inahubiriwa. Wagonjwa wanainuliwa. Vipofu wanaona. Viziwi wanasikia. Pepo wanaghadhabika. Waigaji, Yane na Yambre, wako hapa. Lakini, Mweza yote ananena. Haleluya! Tuko katika siku za mwisho. Tuko kwenye njia panda.

135 "Mioyo ya watu inazimia kwa hofu; mshangao wa wakati; dhiki kati ya mataifa." Dunia inatetemeka sana mpaka inafoka matetemeko ya ardhi kila mahali. Yesu alisema itakuwa hivyo. Kutakuwa na matetemeko ya ardhi mahali mahali. Kuna nini?

Dunia inajua imeamriwa maangamizi. Ina wasiwasi. Ulimwengu una wasiwasi.

136 Lakini Kanisa linapanda katika Injili. Ndivyo ilivyo kwa usalama. "Yeye anijiaye Mimi, sitamtupa nje kamwe." Haleluya! "Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hataingia katika Ufalme." Katika Ufalme, una muhuri wa Mungu wa kibali, Roho Mtakatifu moyoni mwako. Acha mawimbi yapande popote yatakapo. Nyakati zinakuwa mbaya zaidi. Mweza yote anajitokeza. Waigaji wanajaribu kutenda hivyo. Na mambo ya kila namna, wanajaribu kufanya hivi.

137 Nayo Biblia ilisema, yule mwigaji mkuu wa mwisho atainuka kule na kuketi juu ya vilima saba. Atavaa taji yenye sehemu tatu. Naye atatoa nguvu, naye alikuwa na nguvu, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni, mbele za watu. Atafanya hayo yote, hayo yote katika siku za mwisho.

138 Na jinsi ambavyo wangesimama na kuwaiga watu, wakisujudu kwenye makaburi ya wafu, na kila kitu, na kusugua mifupa na kila kitu. Lakini, wakati wakisugua mifupa na kusujudu madhabahuni, Mweza yote anazungumza na mambo ya kimiujiza yanafanyika. Wanasema, "Ni lundo la upuuzi."

139 Lakini Kanisa linakua, miamsho mikuu ya uponyaji ipo kote nchini. Ishara na maajabu yanaendelea kila mahali. Malaika wanawatokea watu. Ishara na maajabu yako hapa. Ni nini, rafiki? Tuko kwenye wakati wa mwisho. Tuko kwenye njia panda. "Inua kichwa chako," alisema, "ukombozi wako umekaribia." Unaona ninachomaanisha? Ni wakati wa njia panda.

140 "Na itakuwa," asema Mungu, "katika siku za mwisho, nitaimwaga Roho Yangu. Wana wenu na binti zenu watatabiri," manabii waliahidi. "Vijana wenu wa kiume wataona maono. Nami nitaonyesha maajabu katika mbingu juu," visahani virukavyo na kila kitu. "Dhiki kuu; nchi itatikisika kwa ninii mbalimbali. . . " Matetemeko makubwa ya ardhi yatakuja, na volkano kubwa zitatokea, na matatizo makubwa, dhiki kati ya ulimwengu. Mataifa yatakuwa yakijaribu kutafuta amani, wakiwa na kisu nyuma ya migongo yao. Kutakuwako na shida kila mahali, mambo haya yote. Nao watu watazidi kuwa wabaya zaidi na zaidi.

141 "Na adui anapokuja kama mafuriko, nitainua kiwango dhidi yake," Roho wa Mungu. Wakati wa njia panda! Mwisho wa safari. Afrika inanguruma kwa mkutano mkubwa wa uponyaji. Na ishara na maajabu yakionekana, kote ulimwenguni, kila mahali. Ni nini? Wakati wa njia panda. Wakati wa mwisho.

142 Magari yasiyo na farasi "yanasongamana katika barabara pana." Mambo haya yote mbalimbali aliyosema. "Mabinti wa Sayuni, jinsi wanavyovalia na kutembea." Jinsi mashoga na mambo mbalimbali yangetokea; jinsi ambavyo, upotovu, "watu

wangeachiliwa kwa nguvu za upotevu," na mambo yote kama hayo. Jinsi wangekuwa "wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wasiopenda kufanya suluhu, wasingiziaji."

143 Na baadhi ya siku hizi, ndugu yangu mpendwa, Yesu atakuja. Na wale wanaojikakamua, katika yale wanayoyaita "ulokole" siku hizi, kuamini katika Injili ya mtindo wa kale ya Kristo, na Mweza yote akizungumza, ya kimiujiza yakitendeka!

144 Yeye alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Katika Jina Langu watatoa pepo, watanena kwa lugha mpya; au wakishika nyoka, au kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." "Mambo haya niliyofanya, nanyi pia mtayafanya. Nitakuwa pamoja nanyi siku zote, hata mwisho." "Mambo haya yatakapoanza kuonekana, inua kichwa chako, ukombozi wako umekaribia."

145 Mnaona, marafiki, kama tu ilivyokuwa katika siku za Nuhu, katika kuja kwake Mwana wa Adamu. Ndivyo ilivyo katika siku za ukombozi wa Israeli. Ndivyo ilivyo kwa Mwana wa Adamu msalabani. Vivyo hivyo na sisi kwenye njia panda. Mungu daima huonyesha ya kimiujiza, hufanya ishara kuu na maajabu, huponya wagonjwa, huwafufua wafu, huwatoa pepo, ile roho kuu ya uamsho; ishara mbinguni, na duniani; dhiki kati ya mataifa. Tuko kwenye njia panda.

146 Jambo linalofuata ni lipi? Yesu Kristo atakuja tena mara ya pili, katika utukufu, kuwapokea wale wote waliokufa katika Kristo na walio hai katika Mungu. Mungu atamleta kila mmoja pamoja Naye. Nao wapole watairithi nchi, nao ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu utaanza. Wala hakutakuwako na vita tena. Watalundika silaha zao, na kufua ninii zao. . . watafua mikuki yao iwe miundu na majembe, na kadhalika. Wala mataifa hayatainua upanga dhidi ya taifa tena. Wala hakutakuwako na magonjwa tena, hakutakuwa na shida tena, hakutakuwa na huzuni tena. Lakini Huko tutaishi, katika Uwepo Wake hapa, milele na milele.

147 Na, ishara hizi zote na kadhalika, tuko kwenye njia panda. Tuko mwishoni mwa safari.

148 Nina furaha sana leo kujua kwamba, katika Kristo Yesu, nimetia nanga nafsi yangu katika mahali pa raha. Nina furaha sana kumwona Mungu, katika Neno Lake takatifu, akifanya na kutoa ishara na maajabu. Na kujua kwamba, leo hii, mbele ya kanisa langu dogo hapa, kwamba ninaweza kusema hivi, kama nilivyofanya hapo awali nilipotokea wakati ule mwingine. Mtauona Uweza mkuu, adhimu wa mwenyezi Mungu katika Nguvu za kimiujiza, zenye uwezo wote, ambazo zitafanya mambo mengi kwa wingi sana, kupita yote ambayo tumewahi kufikiria au kuamini. Na moja kwa moja mlangoni sasa. Nanyi

mnaliona likithibitishwa, moja kwa moja kwenye mlango wa kanisa lenu hapa.

149 Kwa hiyo, maskini marafiki zangu wapendwa, kamwe msimwaibishe Kristo. Mwishieni, kupitia kwa msalaba. Inueni mioyo yenu, na mwinue mikono mitakatifu kwa Mungu. Na kama kanisa, chochote kile, kikianza *hivi*, *vile*, ama watu wakizungumza ama kusema *hivi*, msizingatie hayo. Elekezeni mioyo yenu msalabani pekee na kwa Kristo, na mumwishie Yeye. Mungu na awajalie. Tuko kwenye njia panda, makutano.

150 Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo, kwa ajili ya maombi. Ninataka dada acheze wimbo huu mzuri wa kale, *Imani Yangu Inakutazamia Wewe,* 189. . .-84, tukiwa katika maombi. Nashangaa. . .huku vichwa vyenu vimeinamishwa.

151 Tuko kwenye njia panda, rafiki. Tupo hapo. Mambo haya yote, upotovu huu miongoni mwa wanawake na wanaume, dhiki hii kuu mnayoiona, ni nini? Nimethibitisha hilo kwa Biblia. Imekuwa, kila wakati, ni njia panda. Kamwe haiwi *kabla ya* njia panda; daima ni *kwenye* njia panda. Kabla tu. . .Unaona, watu wameondoka sasa. Walienda kombo kwenye theolojia. "Na siku za miujiza zimepita." Mnaona? Mnaona walifanya hivyo katika kila wakati mwingine.

152 Lakini kabla tu ya wakati wa mabadiliko, Mungu alishuka chini katika uweza yote na kufanya ya kimiujiza. Hiyo ndiyo sababu watu huzungumza kunihusu mimi na kusema mambo wanayosema. Hiyo ndiyo sababu wanazungumza juu ya Wakristo wote wanaoamini hayo.

153 Lakini mnaona kilichowapata kule nyuma, hao walioamini? Walilindwa. Ibrahimu alikuwa salama tu awezavyo. Amina. Na Musa vivyo hivyo; hakuna mapigo yoyote yaliyomsumbua yeye au Israeli. Wala hayakumsumbua Nuhu. Henoko alinyakuliwa kabla halijapata kutukia, akasimama kwenye ngazi za Utukufuni, akiyatazama yakiendelea.

154 Kama uko hapa asubuhi ya leo, bila Kristo, unajua ya kwamba nafsi yako haiko sawa, huku mumeinamisha vichwa vyenu. Laiti ungalifanya hivyo, kwa Mungu. Sijui ni lini nitakapozungumza nanyi tena. Lakini tuko kwenye njia panda. Kama unataka kukumbukwa katika maombi, kwa Mungu, waweza tu kumwinulia mkono wako sasa? Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, bwana. Wewe, wewe. Naam, Mungu awabariki. Wengi wenu, mikono dazani kadhaa.

155 Sasa wakati umeinamisha kichwa chako, tunataka kanisa liuvumishe huu kwa upole. Ukitaka, tuna madhabahu iliyofunguliwa hapa, njoo uombe kidogo tu pamoja nami, kwa Mungu, kwa ajili ya nafsi yako. Nitafurahia kufanya hivyo, kuomba pamoja nawe.

> Imani yangu inakutazamia Wewe, (Si kingine
> chochote ila Wewe.)

Ewe Mwana-kondoo wa Kalvari,
Mwokozi wa Kiungu;
Nisikie sasa ninapoomba,
Ondoa dhambi zangu zote,
Ee niruhusu tangu leo hii
Kuwa Wako kabisa!

Jalia neema Yako tele . . .

156 Je, unaomba? Je, unamwomba akurehemu? Tubu, rafiki mwenye dhambi. Sasa hivi mpe maisha yako.

Itie msukumo bidii yangu;
Kwa kuwa umenifia Wewe,
Ee jalia upendo wangu Kwako,
Uwe safi, wenye joto, na usiobadilika,
Moto ulio hai!

Anapocheza kifungu kingine, na tuwe katika maombi sasa.

157 Baba wa Mbinguni, vema, sisi si kitu, kwanza kabisa, Bwana. Tumekuja tu hapa kwa sababu Wewe ulitunena tukawa. Ulitulisha na kutuhifadhi. Sisi tuliokukubali Wewe, tunashukuru sana, Bwana, kujua hili; kwamba siku moja tutabadilishwa, maskini mwili huu mwovu wa fedheha tunamoishi, utabadilishwa na kufanywa na kufananishwa na mwili Wako. Tunapumzika salama katika safina hii.

158 Na kwa Neno Lako, asubuhi ya leo, kwa Roho Mtakatifu, Yeye amewaletea watu ubao wa kuelekeza. Tuko mwisho, mabadiliko. Ishara na maajabu yanaonekana, mambo makuu yanatendeka. Tunajua, Bwana, ya kwamba tuko mwisho. Hiyo ndiyo sababu vitu hivi viko hapa. Wakati wowote ule, tutamwona Bwana akija.

159 Pia, Mungu, naomba, Wewe ukiijua mioyo ya watu. Ninawapa ahadi hii, mwaliko huu. Wanaweza kuja, Bwana, wamkubali sasa. Ulisema, "Yeye anijiaye Mimi, sitamtupa nje kamwe. Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia hukumuni; tayari amepita akaingia kwenye Uzima wa milele."

160 Ninaomba, Baba, ungeshughulika na mioyo ya watu leo hii. Sio kuwapa ushawishi; ninaamini siku za huo zimepita. Wale wachache tu ulio nao waliosalia, Bwana, hawana budi kuja kwa kiasi, kwa akili timamu, juu ya maungamo yao, wakiamini, wakimkubali Kristo, na kudai kwamba Mungu amekuja mioyoni mwao na kunena. Ninaomba, Mungu, kama umebisha hodi mioyoni hapo awali, kwamba hii itakuwa ni hodi tena leo. Ikiwa ni ya mwisho, itoe, Baba. Neno Lako ni Kweli. Tunaliwasilisha Kwako, sasa, Bwana, kwamba Roho Mtakatifu sasa atashughulika na kila moyo, tunapoimba kifungu cha mwisho.

161 Huku vichwa vyenu vimeinamishwa. Kama unatamani kuja madhabahuni kuomba, rafiki mwenye dhambi, njoo sasa, unapomkubali Kristo. Ama wewe uliyerudi nyuma, njoo sasa hivi na usimame madhabahuni. Tutaomba moja kwa moja pamoja nawe. Vema.

. . .mzingile mweusi wa maisha nimepitia,
(Hivyo ndivyo unavyofanya.)
Na huzuni zimenizunguka, (Mauti, maradhi.)
Bwana, uwe Kiongozi wangu; (Ee Mungu!)
Agiza giza ligeuke kuwa mchana,
Pangusia mbali machozi ya huzuni,
Wala usiniache nipotee
Kutoka karibu Nawe.

162 Huku vichwa vyenu vimeinamishwa. Ndugu Wood, nataka uinue kichwa chako kwa dakika moja. Ndugu Cox, mko humu jengoni, na Ndugu Fleeman? Nataka uinue kichwa chako, ninyi wanaume tu. Mnaona nilichowaambia? "Amin, amin, nawaambia, ya kwamba, nabii katika nchi yake mwenyewe, miongoni mwa watu wake."

163 Sasa, Baba yetu wa Mbinguni, mwenye fadhili, tunauwasilisha Ujumbe huu Kwako, Bwana, kwamba mbegu zilipandwa kwenye kilindi cha mioyo ya watu; kwamba siku moja tukufu, Yesu atakuja, naye atawapata watakatifu wote. Ambalo, atafanya, na kila mtu atanyakuliwa na kupelekwa Utukufuni. Na hiyo itakuwa ni siku ya furaha iliyoje, Yesu Bwana wetu atakaporudi! Tunatambua kwamba tunashukuru sana kuwa tunaishi katika siku hii.

164 Na, Mungu, ninatubia kila kitu, huku nikijua kwamba hatungeweza kuishi kwa nafsi zetu, Bwana, lakini sisi ni—sisi ni wenye dhambi, kwanza kabisa. Nami kila siku, nakutumaini Wewe, nikijua ya kuwa kila siku natenda dhambi, nikijua kwamba mambo ya kila siku yanatokea kwangu na maishani mwangu, ambayo usingependezwa nayo. Nami ninakiri kosa langu na kukukubali Wewe, Bwana Wangu, wakati nafsi yangu mwenyewe imewekwa madhabahuni, asubuhi ya leo, kwenye maskani hii ndogo, imesujudu hapa, Bwana.

165 Ee Mungu, nilikukosea huko nyuma, kwa karama hizo za Kiungu, kama ulivyozionyesha kimwujiza huko ng'ambo, hivi majuzi usiku. Na samahani. Nilitubu Kwako, katika ono. Na sasa katika ninii yangu timamu. . .Katika kiwango hiki ninamoishi sasa, ninatubu Kwako, Bwana wangu, na kukuomba unisamehe, na utanisaidia. Na kwa neema Yako, kwamba umeniambia tayari ya kwamba mambo haya yangetukia wakati ujao sasa. Nikijua kwamba yatatukia, basi, Bwana, naomba kwamba uitakase nafsi yangu na moyo wangu, ninapoukabidhi Kwako.

166 Ee Mungu, usitetemeshe tu nchi, bali na mbingu tena. Bwana, jalia twende hudumani huko, ambako mamilioni

wanangojea, Bwana, na kuona njaa na kiu, na kulia na kuomba, na makafiri wanakufa gizani.

167 Ee Mungu, litikise taifa hili kuu lililoghoshiwa la Marekani, ambalo limeangukia upumbavu, na Sodoma na Gomora mamboleo. "Ewe mwana wa asubuhi, imekuwaje hata ukaanguka?" "Ulipiga mbio vizuri; ulipatwa na nini?" Lakini, Ee Yerusalemu, Yerusalemu, ni mara ngapi Yeye angekuzunguka-zunguka! Na ndivyo ilivyo na Marekani leo hii, kama Roho Mtakatifu anavyolia moyoni mwangu, "Ni mara ngapi ningekufanya kuwa mwenge unaowaka kwa taifa na kwa ulimwengu! Lakini, uliikubali Hollywood, ulikubali mitindo ya ulimwengu. Na sasa umekabidhiwa Yane na Yambre. Na jinsi ninii yako—jinsi siku yako imefika! Jinsi watu wenye nguvu wamelipitia hili taifa, jinsi walivyolichambua kupata kile ambacho wangeweza kupata, na sasa Wewe unajiondoa na kuyaendea mataifa mengine." Ee Mungu, limekaa katika majivu ya magofu yake lenyewe. Limekaa juu ya pipa la madoido yake mwenyewe. Basi siku moja tukufu, Mwana wa Mungu, katika haki Yake takatifu, atafunuliwa kutoka Mbinguni, basi tutasimama wapi?

168 Ee Mungu, utujalie leo kwamba mioyo iimarishwe ndani Yako. Utusamehe dhambi zetu nyingi. Pia, Baba, wabariki wahudumu hawa walio hapa asubuhi ya leo, wahubiri wa Injili. Ee Mungu, jalia watoke leo na Ujumbe huu mioyoni mwao, na kusema, "Ninauona sasa wakati wa mwisho, ubao wa kuelekeza. Nami ninajua tuko kwenye njia panda, na hiyo ndiyo haya yote yanahusu. Nilishangaa ni kwa nini moyo wangu ulikuwa, ulikuwa umesisimkwa sana kwa miaka hii michache iliyopita. Naam, Bwana. Naam, Bwana." Jalia waione.

169 Macho yao na yafumbuliwe, waangalie huku na huku na kusema, "Naam, hii hapa, naona mambo haya yote maovu ni ishara." Ni ishara za ajabu kutoka kwa adui. Mbona, anafanya maajabu makubwa. Anafanya mambo makuu sana, hata kufanya moto ushuke kutoka mbinguni. Naam, wana satilaiti kote duniani. Na—na ni vitu vya asili, adui akileta ishara za moto; na chochote kile, miezi ya uongo na majua ya uongo, na mambo yao mengine yote.

170 Lakini, Mungu, Wewe ulisema kutakuwako na ishara huko juu, pia, ambazo hawatazielewa, nasi tunaishi kuziona. Ninashukuru sana, Bwana, nashukuru sana kwa ajili ya Kristo. Nami naomba ya kwamba Wewe, kwa mtumishi Wako mnyenyekevu. . . Machozi ya toba mashavuni mwangu, Mungu, ninayatoa maisha yangu Kwako, upya leo. Nami naomba unisaidie, Mungu mpendwa, kudumu mnyenyekevu, na kuweka karibu nami watu wanyenyekevu watakaokutumikia Wewe, Mungu mpenzi, nami nitafanya kazi ya Mungu mpaka, Yesu, utakaporuhusu kifo kiniweke huru na maskani hii ya aibu. Na halafu, Baba, ninataka kuwa pamoja Nawe.

171 Libariki kanisa hili dogo la kupendeza. Mungu, mbariki mchungaji wetu mpendwa hapa, Ndugu yetu Neville, rafiki yetu mpendwa anayesimama hapa iwe ni baridi au joto, mambo yawe ni rahisi au magumu, na bado anatangaza Injili hii isiyoghoshiwa ya Bwana Yesu. Mungu, mbariki pamoja na maskini mke wake na watoto. Ee Mungu, jalia aiwashe Injili ndani ya mioyo ya watu, mpaka Yesu atakapokuja. Mbariki. Mungu mpe nguvu nyingi. Tunampenda na tunajua yeye ni mtu mnyenyekevu na anakufanyia kazi. Nami ninashukuru kwa ajili yake, Bwana, kumwachia maskini zizi hi—hili dogo la kondoo hapa, ambalo niliwahi kuwa nalo humu. Na, Mungu, ninaomba tu ya kwamba utamsaidia kuwaleta kondoo wengine wengi zizini. Lijalie.

172 Fanya hivyo kwa kila mhudumu aliyepo hapa. Wala si hapa tu, Bwana, bali ulimwenguni kote, kwa maana tunajua siku hii ina mahitaji. Ishara ziko hapa. Ibilisi ameenda huku na huko, kama simba angurumaye, akishtaki kwa uwongo, na uigaji, na, lakini, Mungu, Wewe unainua bendera dhidi yake, kwa Roho Mtakatifu, nasi tunashukuru. Sasa tubariki, pamoja.

173 Na leo hii, Baba, tunapoenda kuwaombea wagonjwa, naomba umtie mafuta kila mhudumu humu ndani, upya. Tujalie, Bwana. Na jalia kila mwaminio humu ndani atiwe mafuta, na kila mgonjwa apakwe mafuta. Na jalia, tunapotoka hapa, naomba kila mtu apewe afya nzuri kabisa, na utukufu wa Mungu juu ya nafsi zetu, tunapoomba katika Jina la Yesu. Amina.

> Imani yangu inakutazamia Wewe,
> Ewe Mwana-kondoo wa Kalvari,
> Ee Mwokozi . . .

Hebu tuinue mikono yetu tunapoimba.

> . . . Kiungu;
> Sasa nisikie ninapoomba,
> Ondolea mbali dhambi zangu zote,
> Ee nijalie tangu leo
> Niwe Wako kabisa!

Polepole sasa, *Kaa Nami*.

174 Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, tunakabidhi mambo yote Kwako; sisi wenyewe, maisha yetu, ibada yetu. Tutumie sisi sote, Bwana. Jalia kila mmoja aende amevuviwa, leo hii. Jalia hii iwe siku ambayo tutaikumbuka kwa muda mrefu, kwa sababu ya Roho Mtakatifu kuwa pamoja nasi na kutubariki.

175 Sasa wape wagonjwa, Bwana, mahitaji yao leo. Tujalie, Bwana. Utuhurumie, Baba. Fanya hivi kwa ajili ya Yesu, tunaomba.

176 Na sasa, Mwalimu mkuu, ulitufundisha sisi sote, siku moja, uliwafundisha wanafunzi Wako, kama kielelezo kwetu sote, ukasema, "Ombeni hivi:"

Baba yetu uliye Mbinguni, Jina lako Litukuzwe.
Ufalme Wako uje. Mapenzi Yako yafanyike hapa duniani, kama huko Mbinguni.
Utupe leo riziki yetu.
Utusamehe makosa yetu, kama sisi nasi tunavyowasamehe wanaotukosea.
Na usitutie majaribuni, bali utuokoe na yule mwovu. Kwa kuwa Ufalme ni Wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.

177 *Amini Tu*, tafadhali, dada.

178 Ni wangapi wa kuombewa? Je, tunaweza kuona mikono yenu, mnaotaka kuombewa? Sijui kama mngepanga mstari, upande wa kulia *hapa*, wote wawezao. Na wale walio upande *huu*, tungeni mstari kuelekea marefu ya katikati *hapa*, mkiweza. Wale walio kwenye marefu *haya*, fanyeni mstari upande *huu*. Na wale walio kwenye marefu ya katikati, *hapa*. Vema. Hebu tuimbe sasa.

Amini tu, amini tu,
Mambo yote yawezekana, amini tu;
Amini tu, amini tu,
Mambo yote yawezekana, amini tu.

179 Ni wangapi wamewahi kuwa mkutanoni hapo awali, ibada ya uponyaji. Hebu tuone mkono wako. Nyote mmekuwako. Loo, jamani! Mweza yote, mambo ya kimiujiza!

180 Nashangaa. Sasa jambo fulani ndio kwanza linijie, ambalo limebadilisha mawazo yangu kuhusu jambo fulani sasa hivi. Ninaona mstari huu wa maombi labda utatuchukua hadi saa tisa tena, kuumalizia.

181 Yuko wapi Ndugu Tom Merrideth? Bado yuko hapa? Ndugu Junior Jackson? Wote wawili, wahudumu. Ninyi wahudumu, wahubiri wa Injili, mnaoamini katika uponyaji wa Kiungu, njoni hapa kwa dakika moja.

. . . amini tu.

Amini tu, amini tu,
Mambo yote yawezekana, amini tu;
Amini tu, amini tu,
Mambo yote yawezekana, . . . tu.

182 Hebu kidogo, ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Kwa kuwa, Ndugu Cox, na wengi wenu hapa mnajua ya kwamba sehemu hii ya juma, niliwaambia sikutaka ibada ya uponyaji, asubuhi ya leo, hapa. Lakini marafiki fulani waliniita, kwa heshima ya nini? Ndugu Hall alikuwa anafanya uamsho, ibada ya uponyaji, kule kwa Ndugu Durban. Naye Ndugu Hall alikuwa kule. Nilitoa tangazo juma lililopita, kuhusu ibada zake. Ndiyo

sababu ni—nilitoa tangazo hilo, kwa sababu yeye ni ndugu yetu, na anafanya ibada. Na . . .

183 [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Mbona, mbona, Ndugu Hall, huyo ni wewe, Ndugu Hall, hapo? Ndugu Hall yuko pamoja nasi. Vema. Ndugu Hall, unafunga, usiku wa leo, ndugu? Kumbe. Ndugu Durban yuko ng'ambo ya mto. Wana ibada ya uponyaji. Ninamjua Ndugu Hall, ndugu mzuri, mtumishi wa Bwana aliyetiwa mafuta.

184 Sijui, Ndugu Hall, vema, kama haitakuwa ni kuuliza mengi kupita kiasi, unaweza kusimama pamoja nasi, asubuhi ya leo, kwa ajili ya maombi, kwa ajili ya wagonjwa, pamoja nasi? Nachukia kumweka mhudumu, ambaye amekuwa akiomba namna hiyo; kama tu utasimama hapa, na uwepo wako pamoja nasi, ku—kuwaombea wagonjwa.

185 Hebu tuseme, "Mshukuru Bwana kwa ajili ya Ndugu Hall." [Kusanyiko linasema, "Mshukuru Bwana kwa ajili ya Ndugu Hall."—Mh.] Ana ibada kule kwa Ndugu Durban, juma hili. Wengi wenu mumehudhuria, hapana shaka. Nami nilianza kumpenda Ndugu Hall alipokuwa hapa wakati ule mwingine. Na kisha akiwa na mafanikio mengi, Bwana amempa mafanikio makubwa katika kuwaombea wagonjwa. Nami naamini amekuwa hapa kwa muda mrefu, akiwaombea wagonjwa. Na, Ndugu Hall, ungetaka kusema neno kwa hawa jamaa, jambo lolote niani mwako? Vema, bwana. Ulikuwa na mkutano mzuri juma hili, Ndugu Hall? Tumefurahia sana kuwapo kwako hapa.

186 Na sasa ninyi wagonjwa . . . Isitoshe, wahudumu hawa hapa, sote tumejipanga pamoja kama ngome, tukimwamini Mweza yote. Tunaamini ya kwamba Mungu mwenyezi, katika siku hizi za mwisho, anafanya miujiza, na kuwaponya wagonjwa na wanaoteseka, nasi tunaona uwepo Wake wa kila mahali ukifanya vile hasa Yeye alisema angefanya. Tuko hapa kuwaombea asubuhi ya leo. Nami naamini ya kwamba Mungu atafanya jambo hilo.

187 Na hebu kidogo tu. [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Ndugu Jack Oakey, hapa kutoka Kituo cha Uamsho? Mbona, tungefurahi kuwa pamoja nawe, Ndugu Jack Oakey, popote ulipo. Na ndugu yangu amekuja hivi punde tu na kuniambia juu ya Ndugu Jack Oakey fulani. Je, uko humu jengoni? Basi, mbona, wewe—wewe njoo papa hapa pamoja nasi, Ndugu Oakey, popote ulipo.

188 Na wahudumu wengine, mbona, tuna furaha sana kuwa pamoja nanyi. Ikiwa unaamini katika uponyaji, njoo hapa. Huu ndio wito wetu wa kufanya mambo haya, na kuwaombea wagonjwa na wanaoteseka. Hilo ni zuri sana.

189 Ndugu Oakey, wapi . . . Je, huyo ni Ndugu Oakey amesimama hapa pamoja nawe? Hapana. Oakey, Oakey, ninaninii sana . . .

En-he? Wasemaje? [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Vema, mwinjilisti. Yeyote yule, njoo, ndugu mhudumu, moja kwa moja hapa juu, ushirika. Loo, jamani! Hilo ni zuri sana. Njoni moja kwa moja. Jina lako ni nani, ndugu? [Ndugu huyo anasema, "Ndugu Jack Arkly."] Ndugu Jack Arkly. Tuna furaha kuwa nawe, Ndugu Jack, pamoja nasi.

190 Sasa, hiyo ni sawa tu na inapendeza. Ninyi nyote mnaweza kupeana mikono ninyi kwa ninyi, mnapokuja hapo, na kuzoeana.

191 Na sasa hawa ndio Bwana amewatuma kwetu, asubuhi ya leo, kuwaombea watu hawa, na baadhi yao katika hali ya kufa. Yule mama aliyesimama papo hapo nyuma, mwenye kofia nyeupe, ana kansa. Kuna mtu amesimama hapa mbele yangu, ana kansa. Na kuna mambo mengi—mengi mbalimbali. Huyu hapa mwanamke amesimama hapa amevunjika kifundo cha mguu ambacho hakiponi. Tunayo, loo, mambo mengi—mengi hapa. Mama anayeketi hapa mwenye yabisi kavu, kwenye kiti cha magurudumu. Anaamini kwamba Mungu atamruhusu apone. Tunaamini hivyo, pia.

192 Sasa, ndugu, jambo pekee tunaloweza kufanya ni kuomba. Je, hiyo ni kweli? Ombeni tu. Mimi kidogo ni dhaifu sana leo kuingia katika hilo…?…Mnaona, mimi tu…Nilihubiri kwa nguvu.

Kwa hiyo, sasa na tuinamishe vichwa vyetu.

193 Nitawaomba ndugu, ikiwa kila mmoja atakuja. Na kutuandalia mahali papa hapa mbele, hapa, tupate kuwaombea hawa wagonjwa. Nitashuka chini moja kwa moja pamoja nanyi. Nasi tutawaombea wagonjwa, na kuwapitisha wengine, na kuombea kila mmoja. Na kila mmoja wetu aweke mikono juu ya wagonjwa na kuamini ya kwamba Mungu atawaponya. Mnaamini, ndugu? Vipi kuhusu jambo hilo, Ndugu Hall, unaamini hilo kwa moyo wako wote? Vema. Itatendeka.

194 Hebu sasa, kama mkipenda, tutoke nje polepole, chini pembeni, vile vipandio pale, ndugu zangu, mkipenda. Na kutengeneza mstari mdogo pale pale sasa. Nitaanza—nitaanzia hapa chini, nasi tutaomba.

195 Nasi tunataka kanisa lote lijiunge pamoja nasi. Je, mtafanya hivyo, marafiki, tunapowaombea hawa wagonjwa?

196 Sasa, ninyi watu, kuna wainjilisti wazuri hapa, na wahudumu wa miamsho ya uponyaji, walioko hapa kuomba pamoja nanyi asubuhi ya leo. Nasi tuna furaha kugeuza ibada sasa iwe ni ya kuwaombea wagonjwa.

Na tuombe mara nyingine tena.

197 Baba, katika Jina la Yesu, tupokee sasa. Tunamwomba Roho Mtakatifu aje juu yetu na kutubariki, na kutupa kile tunachoomba leo hii. Na nguvu kuu zisizoweza kushindwa za Mungu ziingie ndani yetu sasa hivi. Na Utukufu wa Shekina, Ee

Mungu, ulioishi chini ya mbawa zilizofungamana za Makerubi, na uje chini ya mikono iliyofungamanishwa ya msalaba, na uje juu yetu, leo, Bwana, tunapokuja tukitarajia Nguvu za Mungu. Tunaomba baraka hii kwa watu. Jalia hata mmoja, hata mmoja, asikose, bali kila mmoja na aponywe. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

198 Sasa, Ndugu Neville, kama utachukua mafuta na kusimama mahali hapa sasa, tunapoanza. Hebu na tumwombee mwanamke huyu aliye kwenye kitanda cha wagonjwa, kwanza, kisha chini namna hiyo, halafu turudi nyuma moja kwa moja na kuwaruhusu hao wengine wapite. Vema. Bwana abariki sasa.

Kila mtu katika maombi sasa. Iweni katika maombi sasa.

Vema, ndugu, hapa. Na tuombee uponyaji wake.

199 Baba yetu wa Mbinguni, dada yetu ambaye amelala hapa, atakuwa kwenye kitanda hiki cha wagonjwa maishani mwake mwote. Lakini, tunaamini, Baba, leo, kwa kuwa amekuja hapa kuombewa. Nasi, ndugu Zako, tunaoamini ya kwamba utatufanyia hili, tunaomba kwa unyenyekevu na kuomba katika Jina la Yesu, kwamba umwondolee ugonjwa huu—huu. Mpe kalisi kwa ajili ya mguu huo, mguu wake, au kile kilichovunjika. Nami naomba, aponywe, na ataweza kutembea huku na huko, akimtukuza Mungu. Huku mikono imewekwa juu yake, tunaomba baraka hii katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

200 Baba Mungu, tunaposimama hapa madhabahuni asubuhi ya leo; na huyu, dada yetu mweusi. Tukijua kwamba siku moja, Yesu alipokuwa akiubeba msalaba, kuelekea Kalvari, kule Golgotha, alianguka chini ya uzito wa msalaba. Ndipo mtu mweusi akatokea, akauchukua; akaubeba, akamsaidia kuubeba, akitembea katika alama za miguu za msalaba zilizojaa damu. Huyu hapa mmoja wa binti zake ameketi hapa leo, Bwana, ambaye ameambukizwa, ni mgonjwa, ameketi katika kiti hiki leo hii. Naye angalikuwa hivyo maishani mwake mwote, kama hungemrehemu, Bwana, zaidi ya daktari. Lakini yeye kamwe . . .?. . . Nasi tunaomba . . .?. . . Katika Jina la Yesu, mguu wako upone. Na jalia atembee na aponywe kabisa, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

201 Sasa, wewe, je, unajisikia tofauti . . .?. . . au la? Njoo hapa. Anza tu. Inua miguu yako, ama chochote unachotaka kufanya. Kisha unataka kuwa . . .?. . . useme, “Niliinuka nikapitia mle jengoni.” . . .?. . .

202 Baba yetu wa Mbinguni, ndugu yangu, rafiki yangu, mwenzangu ambaye nimemjua kwa muda mrefu sana, alinipigia simu, hivi majuzi usiku, “Kutafuta, madaktari wananiambia hakuna tumaini.” Nguvu za kansa, ambazo zitayachukua maisha yake.

203 Mungu mpendwa, Wewe wajua moyo wa mtu huyu. Kama kuna jambo lolote kinyume na mapenzi Yako, leo hii, chochote

kile, jalia sasa lisamehewe. Naomba, asubuhi ya leo, saa ii hii, Ndugu yangu Carl anakuja Kwako, na kutoa kabisa, maisha yaliyosalimishwa . . .?. . .

204 Mungu, kama Wewe . . . Madaktari hawawezi kufanya chochote kwa mambo haya. Bali Wewe Ndiwe pekee uwezaye kuyahamisha maisha hayo kutoka hapo, kufanya huo ugonjwa wa kufisha . . .?. . .

205 Na Wewe unayekaa katika utakatifu, Wewe uishiye katika . . . Wewe ndiwe Utukufu wa Shekinah. Wewe ni mwenye nguvu zote. Tunaomba ya kwamba utalitimiza usiku wa leo, kwa ajili ya ushuhuda wa Neno Lako, wa nguvu za Yesu aliyefufuka. Tunaihukumu hiyo kansa, juu ya . . .?. . .

206 Baba Mungu, sasa tunamwombea dada yetu, tukiomba akombolewe kutoka kwa . . .?. . . mateso, na kadhalika. Na sasa, Bwana, tukiomba kwa uaminifu, lakini Wewe utafanya, Kristo yeye yule . . .?. . . Ninaweka mikono juu yake, Bwana! . . .?. . .

207 Mungu mpendwa, tunaweka mikono juu ya huyu, ndugu yetu, ambaye husimama mbele yangu kila siku, maombi yake yalivuka, roho yake ikavuka, naye anatazama kuelekea—kuelekea machweo ya jua. Ee Mungu, vivyo hivyo Ibrahimu naye, akiwa na umri wa miaka mia moja; alinena naye na kusema, "Mimi ndimi El-Shadai." Ee Mungu, Wewe ndiwe mwenye nguvu zote. Nasi tunaomba, Mungu, ya kwamba utafanya miujiza na kumponya huyu, ndugu yetu, katika Jina la Yesu. Amina. Amina. Baba . . .?. . .

208 Baba yetu wa Mbinguni, kama wahudumu wa Injili waliotiwa mafuta, tunasimama leo . . .?. . . Kama kusanyiko lilivyokusanyika katika siku zilizopita, na baada ya Pentekoste walikusanyika na kuomba. Nasi, Baba, tunakusanyika pamoja, kama ndugu waaminio, na watu wote. Nasi tukaomba kwamba hawa watu wakutane; wamekusanyika. Tunaomba aondoke kwa kijana huyu, leo. Naomba asikusumbue tena. Yeye anajua . . .?. . .

209 Baba, tunaweka mikono juu ya dada yetu, na kuomba kwamba, katika Jina la Yesu, ya kwamba utahukumu ugonjwa huu wa mwili wake, na kumfanya mzima kabisa. Wakati anapopitia kwenye mstari huu wa watu, akiweka wakfu maisha yake Kwako, Bwana, akiamini; maisha yaliyoitwa, yakatengwa, na mambo ya ulimwengu, na makanisa baridi, ya kawaida, kuingia katika Injili halisi. Tunaomba katika Jina la Yesu, Yeye ambaye hutoa kulingana na yale tuliyomwomba. Amina.

210 Katika Jina la Yesu, tunaweka leso hii, Bwana, Kwako, na kuombea ukombozi wa binti yake.

211 Baba, tunaweka mikono juu ya dada yetu, anapopitia kwenye mstari huu wa maombi, tukiomba ya kwamba utamkomboa na ugonjwa huu katika mwili wake. Tunapompitisha hapa, tukimwekea mikono, Bwana, takasa

karama pamoja na . . .?. . .Bwana. Lijalie. Katika Jina la Yesu, tunaombea uponyaji wake. Amina.

212 Baba Mungu, tunaweka mikono juu ya dada yetu, tunaomba katika Jina la Yesu. Anapopitia kwenye mstari huu wa wanaume . . .?. . .

213 Baba Mungu, tunaweka mikono yetu juu ya ndugu yetu mdogo, na kuomba katika Jina la Yesu, ya kwamba Wewe utamponya yeyote . . .?. . .

214 Baba Mungu, tunaweka mikono juu ya dada yetu, na kuomba hilo, katika Jina la Yesu, ya kwamba utauponya mwili wake na kumfanya mzima kabisa. Lijalie.

215 Baba Mungu, tunaweka mikono juu ya ndugu yetu, na kuomba katika Jina la Yesu, ya kwamba utauponya mwili huu. Na anapopitia safu hii ya wahudumu, naomba, Mungu, ya kwamba Utukufu wa Shekina utaninii . . .?. . .

216 Ninaweza kuweka mikono juu ya ndugu yetu mwema, mpendwa, na kuomba, anapopitia hapa, kwamba atapitia kwenye Mafuta hayo yanayotakasa, ambayo anaombea.

217 Baba, ninaweka mikono juu ya dada, na kuomba, kupitia Jina la Yesu Kristo, kwamba utamponya na kumpa afya.

218 Baba Mungu, tunaweka mikono juu ya dada yetu . . .?. . . tunapoweka mikono juu yake, katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

219 Baba Mungu, tunaweka mikono juu ya ndugu yetu . . .?. . . magonjwa, Bwana.

220 Aminini sasa, wanapopita. Wametiwa mafuta, kama Neno lilivyofundisha.

Katika Jina la Yesu . . .?. . .

221 Baba Mungu, tunaweka mikono juu ya dada yetu, Bwana, anaposhuka kwenye mstari huu. Katika . . .?. . . shauku ya moyo wake . . .?. . .

222 Baba Mungu, tunaweka mikono juu ya ndugu yetu, na kuombea uponyaji wake.

223 [Mstari wa maombi unaendelea kwa dakika tatu na sekunde kumi na tano, mengi ya maneno ya Ndugu Branham hayatambuliki—Mh.]

224 Je, ulipata kugundua, ajabu? Nilihubiri asubuhi ya leo, juu ya "barabara za makutano." Angalieni njia panda hapa . . .?. . . safu hii ya wanaume.

225 [Mstari wa maombi unaendelea kwa dakika sita—Mh.]

226 Ee Mungu, Mweza yote! Lijalie, Bwana, ya kwamba Roho na nguvu zitakuja juu ya dada yetu, kumfanya mzima kabisa. Tunaomba, katika Jina la Yesu, anapowapitia wahudumu hawa, na awe mzima kabisa usiku wa leo. Amina.

227 [Mstari wa maombi unaendelea kwa sekunde arobaini na tano—Mh.]

228 Baba, katika Jina la Yesu, tunaombea leso hii, sawa na ile iliyochukuliwa kutoka katika mwili wa Paulo. Nami naita. . .?. . .Omba, Mungu, kwamba aponywe, asubuhi ya leo, katika Jina la Yesu. Amina.

229 Mpendwa, rafiki, katika Jina. . .Ngoja, huyu hapa mama mmoja anakuja kuombewa. Naam, njoo papa hapa juu. Ninyi ndugu. . .

230 Baba yetu mpendwa wa Mbinguni, tunaweka mikono juu ya dada yetu. Nasi tunashukuru sana kwamba anapata nafuu. Imani yake na isilegee sasa. Na. . .?. . .katika Jina la Yesu Kristo. . .?. . .

231 Sasa tumefanya nini? Alichokisema Bwana. Je, hiyo ni kweli?

232 Tuna furaha kuwa pamoja na ndugu zetu wahudumu, wanaotutembelea, marafiki hawa wote. Semeni, "Amina," nyinyi nyote ambao. . .[Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, bila shaka mnakaribishwa tena, ndugu zangu wapendwa, kuwa pamoja nasi. Na leo hii, karibu tu tutafaulu, ku—kutoka kwenye wakati ufaao. Tuna furaha mlikuwa hapa. Na, ndugu zangu, ninawaombea ninyi kila mara. Nanyi mniombee, popote mwendapo, na muombe sasa ninapoenda hudumani tena. Njia zetu na zikutane, wakati baada ya wakati.

233 Kumbuka, Ndugu Oakey, huenda mimi. . .Ilitokea niliwakumbuka wapendwa wake huko nje Ca—California. Je, huyo ni Dk. Oakey, wa. . .? [Ndugu Oakey anasema, "Hapana."—Mh.] Loo, Oakey yule mwingine. Naam, bwana. Nami—nami najua kuna Oakey wengi huko nje. Sikujua tu alikuwa na uhusiano na yupi. Ninamjua Dk. Oakey, yule daktari wa meno, unajua. Halafu, na—na kwa hiyo. . .Je, wewe ni jamaa yake, pia? ["Yeye ni binamu yangu."] Binamu yako. Vema, hilo ni zuri sana. Mtu mzuri!

234 Sasa, tumewafanyia nini ninyi watu hapa? Jambo ndilo hili. Hatungesimama hapa na kuweka mikono juu ya wagonjwa isipokuwa tuliuamini. Tumewaona watu waliotuzunguka leo, wanaoketi kwenye kusanyiko hili papa hapa; hao watu wameugua kansa, vipofu, vilema. Hebu tu niwaonyeshe jambo fulani, kama kuna wageni hapa. Ni wangapi hapa ambao wameponywa, kwa njia hiyo, na Mungu? Hebu tuone mikono yenu ikiinuliwa. Hao ni, vipofu, kansa, na chochote kile, mnaona. Mnaona? Atakufanyia vivyo hivyo. Unaona? Sasa, tunafanya, hivi: tunaamini maombi yetu.

235 Na sasa kwenye la kumalizia, kabla hatujairudisha ibada kwa Ndugu yetu Neville, kumbukeni ibada usiku wa leo. Na usiku wa leo, ikiwa kuna mtu yeyote ambaye—ambaye unajua, mpendwa ambaye hajaingia asubuhi ya leo kuombewa, Ndugu Hall, hapa, yuko kwa Ndugu Durban. Na hiyo itakuwa. . .Na

anwani ni ipi, ndugu? [Ndugu mmoja anasema, "Sijui anwani."—Mh.] Ati nini? [Ndugu mwingine anasema, "Ya kumi na saba na Soko."] Ya kumi na saba na Soko, huko Louisville, ambapo wana uamsho wa uponyaji. Na hiyo ndiyo ilikuwa sababu hasa nilisita kuhusu kufanya ibada. Si—si—sipendi kwenda mahali ambapo mtu anafanya u—u—uamsho wa uponyaji, kisha mtu anaanzisha mmoja. Na hiyo ndiyo sababu nilisema kuhusu kutoninii... kuhusu ibada asubuhi ya leo, ni kwa heshima ya Ndugu Hall kwa Ndugu Durban, maana wote wawili ni marafiki zangu wapenzi sana.

236 Wala hatutaki uamsho wa uponyaji uendelee hapa, wakati Ndugu Hall anao mmoja unaoendelea kule. Nina hakika na hilo. Na, kwa hiyo, tunampenda.

237 Na sasa, Ndugu Oakey, uko wapi, ndugu? [Ndugu Oakey anasema, "Soko la Arobaini-thelathini la Magharibi."—Mh.] Soko la Arobaini-thelathini la Magharibi. Huyo ndugu mwingine aliye nawe hapo, mko pamoja? Vema. Sasa hiyo ni kwenye la thelathini...arobaini...["Soko la Arobaini-thelathini Magharibi."] Soko la Arobaini-thelathini, arobaini-thelathini Magharibi, Louisville, uamsho mwingine. Na kwa hiyo utakuwa pale kwa muda gani, Ndugu Oakey? ["Nitahubiri huko juma zima."] Juma hili lote lijalo. Hilo ni sawa. Sasa, ninyi nyote mlio wagonjwa, thelathini... arobaini, Soko la Magharibi. [Kusanyiko linasema, "Soko la Arobaini-thelathini Magharibi."] Naam. Arobaini na moja kwenye Soko la Magharibi. Vema. Hilo ni sawa. Sasa ipo...

238 Niliona wahudumu wengine kadhaa. Ndugu hapa, una uamsho unaoendelea mahali fulani, bwana? La. La. Naam. Vema, hilo ni zuri sana. Hiyo ni sawa.

239 Na huyu ndugu hapa ni m—mmishenari kwa Wayahudi, ninaamini, sivyo? Na mmishenari kwa Wayahudi. Nafikiri anaishi New Albany. Na kwa hivyo tuna furaha sana kuwa na...

240 Je, nilikosa mmoja? Je, kuna mtu mwingine mahali fulani? Na—natumaini sikumkosa; sikusudii. Bila shaka, Ndugu Junior Jackson, mnajua mahali aliko huko New Albany.

241 Ndugu Tom Merrideth ana matangazo. Je, una kanisa, Ndugu Merrideth? Hana kanisa. Ni tangazo tu. Alilitangaza, dakika chache zilizopita.

242 Naye Ndugu Neville amekuwa na ibada hapa kwa ajili yenu ninyi watu hapa, karibu na hapa, usiku wa leo, na kwa ajili ya Jumatano hii ijayo, na juma zima. Na i—ibada zake, matangazo yake, ni Jumamosi asubuhi. Vema.

243 Kila mtu anajisikia vizuri? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, marafiki. Inakufanya utake kujiunga na kundi hili zuri, lenye furaha la wahubiri, na kwenda kuihubiri Injili, na kuwaombea wagonjwa, pia. Mungu awajalie ninyi, marafiki.

244 Yule kijana mwananmume pale aliyetupwa kutoka kwenye ajali ya barabarani hivi majuzi tu, kipande cha chuma kilipitia ubavuni mwake, kikapitia ndani yake, na kutokea upande wa pili, namna hiyo. Mama mpendwa, mwombaji! Mungu alimhifadhi kwa kusudi fulani. Kwa kuwa aliniambia, niliwazia. . . Asubuhi ya leo, nilikutana naye nikija ukumbini. Alinipa mkono. Nikasema, "Wewe si ni yule mvulana?"

245 Akasema, "Naam, bwana." Kasema, "Aliyeitwa hudumani." Mungu aturehemu! Sasa, ndugu zangu wapendwa. . . Kijana mwanamume tu, ameketi pale amevaa koti ya kahawia. Mungu na ajalie kwamba atakuwa nuru inayowaka, tukiwa kwenye makutano ya barabara, mwanangu. Na, ahubiri Injili, ahubiri Injili yote, ahubiri Neno lote la Mungu, wala asipatane hata kidogo. Asimame pale pale kwenye wajibu wake. Mungu atakufanya shujaa hodari.

Sasa, hebu na tuombe ombi hili moja la mwisho sasa kwa ajili ya wagonjwa.

246 Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe kwa ajili ya kijana mwanamume huyu, asubuhi ya leo, pia, Bwana. Naye anapoketi pale asubuhi ya leo, akisikiliza Neno, na kuwaona wahudumu hawa huku mioyo yao ikiwaka moto, walipoweka mikono juu ya wagonjwa, walipokuwa wakipitia kwenye mstari huu. Wakiona shuhuda pale, za watu wakiinua mikono yao, ambao wameponywa kansa, na upofu, na viziwi na bubu, na viwete. Ni—ni changamoto. Nasi tunalitazama Neno hili kuu lililobarikiwa, nalo lilisema siku hizi zitakuwa hapa, nasi hawa hapa tumesimama. Tunamwona Mungu mwenye nguvu zote akiwa ameunyosha mkono Wake, na ishara na maajabu yakija. Tunasikia sauti ya mvua tele angani. Tunajua ya kwamba tuko katika siku kuu ya mvua ya mwisho.

247 Wakati, Shetani atafungwa na kutupwa shimoni, amefungwa kwa mnyororo wa hali ya mambo, asiweze kutoka na kuwadanganya mataifa tena. Na miaka elfu moja, ule Utawala wa Miaka Elfu, utafanyika duniani wakati tukimtukuza Bwana wetu Yesu, na kumpamba; kumvika taji, "Mfalme wa mfalme, na Bwana wa mabwana."

248 Maskini dunia hii yenye dhambi itapasuka, moja ya siku hizi, hapo nguvu za atomiki zitakapoachiliwa, na haidrojeni iachiliwe. Na kila bahari, na maji, yataninii. . . Bahari itavuma hadi ikauke. Ee Mungu! Na jua litashindwa kuangaza. Na mwezi hautatoa mwanga wake. Na nyota za mbinguni zitaanguka kama vile mtini upukutikishavyo mapooza yake utikiswapo na upepo mwingi. Na watu wataililia miamba na milima. Basi maisha haya madogo yatakuwa na faida gani?

249 Ndipo waliokufa katika Kristo watafufuka. Loo, paradiso iliyoje! Mataifa hayatainua upanga juu ya taifa lingine, tena. Wala hatutakuwa na mstari wa maombi kwa ajili ya wagonjwa.

250 Leo ndiyo siku ya wokovu. Na, Baba, tuliwaleta watu hawa Kwako. Nasi tumekuomba, katika Jina la Yesu, Yule aliyesema hivi, "Mwombeni Baba lolote katika Jina Langu, litafanyika." Sasa, sisi, si maombi yetu tunayoamini. Ni agizo Lake, ndilo tunaloamini. "Mwombeni Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya."

251 Sasa, Shetani, wewe ambaye umekuwa mwovu sana, na umewafunga watu hawa, na kuweka mauti juu ya wengi wao, na kuwalemaza, na kuwapofusha, na kuwafanyia kila aina ya uovu, umeshindwa. Umeshindwa, kwa sababu tumefanya tu vile Yesu alivyosema tufanye. Kwa hiyo, imani yetu inaangalia sasa na kukwambia, "Waache watu hawa. Toka ndani yao, katika Jina la Yesu! . . .?. . . Na hebu kila mmoja awe mzima, kupitia Jina la Yesu Kristo.

Bwana asifiwe! Sasa aminini.

Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini;
Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini;
Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini
Kwamba Yesu ananiponya sasa.

Ninamkubali katika Neno Lake;
Ninamkubali katika Neno Lake;
Ananiletea ukombozi bure,
Ninamkubali katika Neno Lake.

Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini;
Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini;
Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini
Kwamba Yesu ananiponya sasa.

252 Je, huliamini? Kwa moyo wangu wote! Ndugu Saul, unaliamini? [Ndugu Saul anasema, "Amina."—Mh.] Unaamini ya kwamba Mungu atafanya hilo, Ndugu Tony? [Ndugu Tony anasema, "Amina."] Amina. Dada Snyder, unaamini? [Dada Snyder anasema, "Amina."] Dada, *wewe* unaamini? Je, *wewe* unaamini, dada?

253 "Na imani ni hakika ya mambo yatarajiwayo, bayana ya mambo yasiyoonekana." Kwa imani tuliona zile kuta kubwa za Yeriko zikianguka! Kristo hukuongoza kwa imani. Je, unaamini hivyo? Amina. Tunaamini. Kamwe msiwe na kivuli cha shaka, kamwe. Mungu atalimaliza. Mweza yote! Ni hakika kabisa! Inabidi tu kulifuata. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Amina. Yeye si ni wa ajabu?

254 Sasa, na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi ya kufumukana. Tutaomba . . . Tutazunguka-zunguka pamoja, kwa muda kidogo wa ushirika. Tutaomba kama Ndugu Neville, kama atakuja hapa sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu sote katika maombi mafupi. Tunapovumisha kwanza, huku vichwa vyetu vimeinamishwa:

Ninaweza, nitaamini, kweli ninaamini;
Ninaaweza, nitaamini,. . .

255 Kumbuka tu, Yeye yuko moja kwa moja kando yako. Yupo kulifanya halisi. Hisi tu Nguvu Zake zikiingia ndani yako sasa. “Naweza?” Hakika, unaweza.

Nitaamini Neno Lake;
Nitaamini Neno Lake;
Hunileteea, ukombozi bure, (Pale Kalvari.)
Nami nitaliamini katika Neno Lake.

256 Tunapoinamisha vichwa vyetu sasa. Ndugu Neville, pamoja na yale unayotaka kusema.

56-0115 Njia Panda Ya Wakati
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org